**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Saba – Tarehe 8 Februari, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika* (*Mhe. Job. Y. Ndugai*) *Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Taarifa ya Mwaka ya Utendaji wa Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2010/10/2011 *(The Annual Performance Evaluation Report of Public Procurement Regulatory Authority for the Financial Year 2010/2011).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 81

**Tatizo la Maji Kwenye Vijiji vya Jimbo la Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Vijiji vyote vya Jimbo la Kalambo vilivyo katika mwambao wa Ziwa Tanganyika katika Tarafa ya Kasanga na vile vya Mambwekenya, Mpanga, Madhibita na Kazonya vinakabiliwa na upungufu mkubwa wa maji na hata vile vilivyopata ufadhili wa Benki ya Dunia, hakuna hata kimoja kilichofaidika na ufadhili huo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuhakikisha adha hii ya maji inaondolewa katika vijiji tajwa kwa kuzingatia uwezo mdogo wa Halmashauri ya Sumbawanga?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba lipo tatizo la upatikanaji wa maji katika vijiji vya Jimbo la Kalambo. Kwa kuzingatia kero hizo, Serikali kupitia uhisani wa Benki ya Dunia inatekeleza mradi wa maji katika Vijiji vya Mwimbi, Mwazye, Kamawe, Kisomba Kasote na Matai vilivyopo katika Jimbo hilo na ambavyo vitatumia teknolojia ya maji ya mtitiriko *(Gravity Scheme)* isipokuwa Kijiji cha Mwimbi ambacho kimechimbiwa kisima kirefu cha maji.

Halmashauri imeshapata kibali cha kutangaza zabuni ya kupata mkandarasi atakayejenga miundombinu ya maji ili huduma hiyo ianze kutolewa kwa wananchi. Fedha zilizotumika kutekeleza mradi huu zilitokana na bakaa ya Bajeti iliyokuwa imeidhinishwa ya mwaka 2009/10 sawa na shilingi milioni 40.74.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga katika Bajeti yake ya mwaka 2011/2012 imetenga shilingi milioni 976,698,000 kupitia programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini kwa

ajili ya kujenga miundombinu ya maji katika vijiji 10 vinavyotekelezwa miradi ya maji vikiwemo Vijiji vya Kalambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Mambwekenya, Mpanga, Madhibita na Kazonya na baadhi ya vijiji katika Tarafa ya Kasanga, havikupata kipaumbele cha kuingizwa kwenye utekelezaji wa programu ya maji kutokana na kushindwa kukidhi kigezo cha uchangiaji ambacho ni asilimia 2.5 ya gharama za mradi.

Aidha, vijiji ambavyo havikupata maji baada ya kuchimbiwa visima vitaingizwa katika awamu ya pili ya utekelezaji wa *program* ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a)Kwa kuwa wimbo kuhusiana na Benki ya Dunia katika kusaidia kuleta maji imekuwa ni wimbo wa muda mrefu sana na kwa kuwa katika Jimbo la Kalambo na hususan Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga hakuna hata kijiji kimoja ambacho kilishafaidika mpaka ninavyoongea leo na kwa kuwa tatizo kubwa limetokana pia na kutokuwepo na Mhandisi yuko *technician*.

Je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba inasaidia Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kupatiwa Mhandisi? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa kila inapofika kipindi cha masika mwambao wa Ziwa Tanganyika hukumbwa na magonjwa ya matumbo kwa ajili ya kukosekana kwa maji salama. Je, Serikali iko tayari kushirikiana na Mfuko wa Ziwa Tanganyika kuhakikisha kwamba vijiji vyote vya Ziwa Tanganyika vinapatiwa maji kwa sababu vina vyanzo vizuri sana na Halmashauri haina uwezo wa kuhakikisha maji safi na salama yanapatikana? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Kalambo kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, naomba wananchi wa Sumbawanga waelewe kwamba utekelezaji wa mradi huu wa vijiji 10 unakwenda kwa hatua, hatua ya kwanza ni ya usanifu, halafu tukishakamilisha tunaanza kuchimba visima, baada ya hapo tunaendelea na kujenga miundombinu.

Sasa katika utekelezaji ambao umeshafikiwa mpaka sasa tayari visima vinne vimeshachimbwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na hatua inayofuata sasa hivi ni kujenga miundombinu na shilingi milioni 900 ambazo zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Sasa suala linakuja kwamba vijiji anavyovitamka Mheshimiwa Mbunge havikuwa vimewekwa katika ile awamu ya kwanza ya vijiji 10. Sasa naomba sana Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kwamba katika awamu itakayofuata ya *program* vile vijiji anavyovizungumzia Kando ya Ziwa lile viwekwe kwenye awamu ya pili na uchaguzi ni vijiji vipi ni Halmashauri inayochagua. Kazi ya Serikali ni kuratibu na kuweza kusimamia utekelezaji wake. Kwa hiyo, kazi imeshafanyika ijapokuwa siyo kwamba vijiji vyote 10 walivyochagua vimeshapata maji. Lakini tuko kwenye hatua ambayo inaendelea vizuri.

Kuhusu suala la udhaifu wa mtalaam naomba nimwahidi kwamba tutalifuatilia na kuangalia tupate watalaam ambao kwa kweli wanaweza kufanya kazi ambazo zinaonekana. Serikali itafuatilia na tutashughulikia suala la mtalaam kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.

**MHE. MOSES JOSEPH MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa miradi mingi ya maji ambayo inategemea ufadhili wa Benki ya Dunia unaonekana kusuasua na hivyo kupelekea hata wakazi wa Jimbo la Kasulu Mjini Mkoa wa Kigoma kukabiliwa na tatizo la maji hasa katika vijiji kama vya Elujuu na vyanzo vya maji tunavyo. Je, Serikali ina mkakati wa kuhakikisha tunaweza tukapata fedha nyingine ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu hawaendelei kukumbwa na adha ya maji badala ya kuendelea kutegemea miradi ya Benki ya Dunia ambayo inaonekana kusuakusua na kulegalega katika maeneo mengi ya nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Machali, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa miradi hii ya *World Bank* inasimamiwa na Halmashauri na Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri yake. Sasa hatua zile ambazo zinaendelea kwa mfano ni vizuri na ninyi mkawa mnafuatilia ili kusudi msaidie Serikali katika udhibiti wa uendeshaji wa miradi hii.

Sasa tukisema tu kwa ujumla inasuasua wakati sehemu zingine wamefanya vizuri kweli kuna Wilaya zingine ziko nyuma. Lakini baadhi ya Wilaya zimekwenda mbele kwa sababu ya ufuatiliaji wa karibu pia pamoja na Madiwani pia na Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge uwe karibu sana na Halmashauri ya Wilaya katika kufuatilia utekelezaji wa miradi hii. Sasa suala la kwamba kama tunatafuta fedha zingine maana tumekubaliana katika *program* kwamba nguvu zote tuzikusanye pamoja lakini *World Bank* ndio wanaongoza katika kusimamia.

Sasa tutakapoona kwamba tuna matatizo na *World Bank* tunaweza tukaangalia njia nyingine ambazo tunafikiri tunaweza tukafanya vizuri zaidi hapo baadaye.

Na. 82

**Sheria Inayowalinda Wafanya Usafi Barabarani**

**MHE. LUCY T. MAYENGA (K.n.y. MHE. MARTHA MOSES MLATA)** aliuliza:-

Je, ni sheria gani inayowalinda na kuwatambua wafagiaji wa barabara na maeneo mengine nchini ili kuweka barabara na miji safi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inayowalinda na kuwatambua wafanya usafi barabarani ni Sheria ya Afya na Usalama Kazini Namba 3 ya mwaka 2003.

Sheria hiyo inatoa kinga kisheria kwa wafanyakazi au mtu yeyote anayefanyakazi za usafi barabarani katika miji na maeneo mengine ndani ya mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inatoa masharti kuwa wafanyakazi wanatakiwa kuwa na vifaa maalum vya kujilinda na majanga mbalimbali yakiwemo ya ajali na magonjwa wakati wanafanya usafi. Vifaa hivyo ni pamoja na makoti ya kuakisi mwanga *(reflectors) Gumboot, gloves* na *masks*, alama za barabarani kuonyesha kuwa kuna watu wanaofanya usafi au kazi za usafi zinaendelea na alama zingine ambazo hutambulika kimataifa kwa mujibu wa sheria ya usalama barabarani na. 30 ya mwaka 1973. *(Makofi)*

Ni wajibu wa vikundi na makampuni yanayojishughulisha na shughuli za usafi kuhakikisha wafanyakazi wao wanapewa vifaa husika na vinatumika ili kuwahakikishia usalama wafanyakazi hao wawapo kazini.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vitendea kazi hivi havitolewi kama ambavyo inatakiwa vitolewe na makampuni makubwa pamoja na madogo ambayo yamekuwa yakipata tenda mbalimbali za kufanya usafi katika maeneo mbalimbali kwenye Halmashauri zetu na kadhalika zimekuwa hazitendi haki kwa kuwapa ujira mdogo sana.

(a)Je, Serikali iko tayari kuweza sasa kuingilia kati kwenye ngazi ya Halmashauri kutoa agizo ili Watanzania wenzetu hawa ambao wanafanya kazi kwenye mazingira magumu mazingira yao yaweze kuboreshwa?

(b)Kwa kuwa vile wafanyakazi hawa wamekuwa wakifanya kazi hizi ambazo zimekuwa wakati mwingine ni *risk* kwa maisha yao kwa maana ya kwamba wamekuwa wakifagia barabara nyakati za mchana.

Je, Serikali haioni kwamba kazi kama hizi sasa hasa katika Jiji la Dar es Salaam zingetakiwa kufanywa ikiwezekana nyakati maalum za usiku kwa ujira mzuri ili kuepusha *risk* zao na hatari zao hasa wakati ambapo baadhi yao wamekuwa wakipata ajali na kadhalika? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lucy Mayenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tuweze kuelewana kwamba tunafanya nini ile sheria ambayo nimei-*quote* hapa ina-*commit* miji kwamba ifanye kazi hii ambayo tunaizungumza hapa.

Lakini utaratibu ambao unafanyika hapa ni ule wa *PPP* kwamba kuna *Private Public Partnership* kuna Halmashauri inachofanya pale ni kwamba inaiagiza ile kampuni ambayo ndio inatoa *service* hiyo ifanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Mbunge, anachosema kama Halmashauri yenyewe ndio inayofanya basi Halmashauri yenyewe nayo inatakiwa itoe vile vifaa ambavyo nimevitaja hapa.

Kama ni kampuni ambayo imekuwa *outsourced* imepewa kufanya kazi hiyo kinachotakiwa hapa ni kwamba kwa maana hii anayozungumza ni kwamba Halmashauri lazima pia i-*take interest* kwa kifupi hapa ninachoweza kusema ni kumwambia yule mtu ambaye ninakupa kazi au mimi sitakupa kazi. Kwa sababu wale wanaofanyakazi pale ni wananchi wanaotoka kwenye Halmashauri ile na *interest* ya Halmashauri pia ni kuhakikisha kwamba hawa wafanyakazi wanaofanya kazi pale, wanakuwa na hivi vifaa tunavyosema hapa.

Kwa maneno mengine au kwa kifupi ninasema hivi kama mfanyakazi wako hutumii vifaa hivi sitakupa tena kazi wewe. *(Makofi)*

Kwa nini, nimekuta watu wangu wanafanya kazi pale, magari yanawagonga pale. Kwa hiyo, sikupi kazi tena kama ukifanya hivyo tena itakuwa ni *violation* ukienda kwenye OSHA wale *operation levy* wanasaini mkataba pale wanasema kwamba vifaa vyote vitapatikana. Amenitaka mimi hapa niseme kwamba wafanyakazi hawa ambao wana risk maisha yao wanafanyaje hili usiku ukienda *Chicago, New Dell* ukienda mataifa makubwa makubwa haya hawafanyi kazi hizi asubuhi wanafanya usiku kabisa.

Kwa hiyo, hili tunalichukua hapa tutalifanyia kazi tutazungumza na Halmashauri zetu tuone uwezekano huo wa kufanya hivyo. Lakini hili ambalo hawatumii vifaa hivyo ambalo kwa niaba ya Serikali ninasema Halmashauri husika waweze kuhakikisha kwamba hawa watu wanafanya kazi na vifaa hivyo vinatumika.

Kama havitumiki tutachukua hatua maana yake ni kwamba makampuni yale tutakwenda kufuta mikataba. *(Makofi)*

Na. 83

**Matumizi ya Kifaa cha Asycuda ++**

**MHE. ZAHRA ALI HAMAD** aliuliza:-

Serikali iliamua kutumia kifaa cha ASYCUDA ++ ili kuondoa tatizo la tofauti ya ulipaji wa ushuru wa forodha iliyokuwepo kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

(a) Je, chombo hicho kimefanikiwa kwa kiasi gani mpaka sasa?

(b) Je, ni kwa nini mpaka sasa tatizo hilo halijatatuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zahra ali Hamad (Mbunge wa Baraza la Wawakilishi) lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, *ASYCUDA++* ni Mfumo wa Kompyuta unaotumika na kuboreshwa ndani ya mfumo mpya wa ukadiriaji wa thamani za bidhaa kutoka na kupelekwa nje ya nchi uitwao *Imports and Exports Commodity Data Base (IECDB).*

Mfumo huu ulianzishwa Tanzania Bara mwezi Aprili, 2010 na kwa sasa ukadiriaji wa kadhia zote bila kujali mali itaingia kituo gani cha forodha, unafanyika katika kituo cha huduma za forodha Dar es Salaam *(Central Data Processing Office)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu umeweka usawa katika ukadiriaji wa kodi kwenye bidhaa kutoka nje na kuongeza ufanisi ikiwa ni pamoja na kuzuia uvujaji wa mapato ya Serikali. Mfumo huu umeiwezesha Mamlaka ya mapato kufanya ukadiriaji wa kodi unaofanana nchi nzima.

Vile vile, mfumo huu umeboresha utunzaji wa kumbukumbu na takwimu za kibiashara kati ya nchi yetu na nchi nyingine duniani. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la tofauti ya ushuru kati ya Zanzibar na Tanzania Bara litapata ufumbuzi wa kudumu pale Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakaporidhia na mfumo nilioutaja ambao utaondoa tofauti ya ukadiriaji wa ushuru wa forodha kati ya sehemu hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Tanzania Zanzibar bado inatumia mfumo wa *ASYCUDA++* pekee na haukuunganishwa na mfumo wa *data base* nilioutaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa kuzingatia kuwa bandari za Zanzibar ni vituo muhimu vya forodha vya kuingizia bidhaa nchini Tanzania. Wizara yangu inaendelea kushauriana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili ijiunge na mfumo huu mpya. *(Makofi)*

**MHE. ZAHRA ALI HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake marefu na ya ufasaha na pia nina swali la nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni kuwa manung'uniko na manung'uniko haya yataendelea kuwepo kwa muda mrefu kwa sababu mfumo wa kodi unaowekwa unahusu nchi mbili zenye chumi mbili tofauti?

(b) Kwa kuwa uwezo wa kiuchumi wa watu wa Zanzibar ni mdogo. Je, Serikali haioni kuwa ni busara viwango vya kodi vikawekwa tofauti? Nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Tanzania Bara na Zanzibar ni chumi mbili lakini tusisahau ukweli kwamba ni soko moja. Kwenye soko moja hutaweza kutofautisha ushuru.

Kwa hiyo, kinachoweza kufanyika ni kuendelea kufanya mazungumzo tuangalie tunaweza tukasaidiana vipi kwenye chumi zetu lakini siyo kutofautisha ushuru.

Lakini lingine ni kwamba tukumbuke kwamba Tanzania imejiunga na soko la pamoja la Afrika Mashariki na Ushuru wa Forodha. Chini ya taratibu hizi hakutakiwi kuwe na tofauti hizi za kiushuru.

Lakini kunaweza kukawa na njia za *compensation* ambazo zinaweza zikasaidia kuweka *balance* ambayo inatakiwa katika ukuaji wa chumi hizi. *(Makofi)*

Na. 84

**Mauaji ya Ng'ombe**

**MHE. SAID AMOUR ARFI (K.n.y. MHE. ANNA M. J. MALLAC)** aliuliza:-

Kuna ushahidi kuwa askari wa wanyamapori *(TANAPA)* wameuwa ng'ombe 56 katika Vijiji vya Ikiba, Kishishi na Chamaledi, Wilaya ya Mpanda, Tarafa ya Mpimbe:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhusu jambo hilo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuwafidia wafugaji hao waliopata hasara hiyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Anna Marystella J. Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) napenda kwanza nitoe pole kwa wananchi wa maeneo hayo kwa taarifa hizi ambazo ziko kwenye swali, lakini pia naomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo:-

Eneo la Hifadhi ya Taifa ya Katavi imezungukwa na pori la Akiba la Rukwa-Rukwati na Lwafi, pamoja na mapori tarajiwa ya Hifadhi za Jamii ya Ubende na Mpimbwe. Maeneo hayo yote ni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na ushahidi wa kuwepo kwa wimbi la kuzagaa kwa silaha katika Mikoa ya Rukwa na Kigoma ambapo wananchi wasio waaminifu wanamiliki silaha kiholela na kuzifanyia ujangili, ujambazi na uhalifu wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo mafupi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Marystella J. Mallac, kama ifuatavyo:-

(a) Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* kupitia Hifadhi ya Taifa ya Katavi haijawahi kupokea malalamiko au madai yoyote yanayohusiana na mauaji ya mifugo yaliyofanywa na askari wake.

Aidha, tuhuma za mauaji ya mifugo ni moja wapo ya mashauri ya jinai ambayo mlalamikaji anatakiwa kupeleka mashitaka polisi ili uchunguzi huru ufanyike kubaini ukweli wa jambo hilo na watuhumiwa kuchukuliwa hatua.

(b) Hadi sasa Shirika la Hifadhi *(TANAPA)* haliwezi kulipa fidia yoyote kwa jambo ambalo halijathibitika kisheria kuwa limefanywa na watumishi wa *TANAPA*.

Hata hivyo Wizara yangu itafuatilia kwa karibu suala hili kwa kina kwa kushirikiana na vyombo vya dola ili kubaini ukweli wa jambo hili na kujiridhisha juu ya ukweli wa tuhuma hizi na kuweza kusaidia kuchukuliwa kwa hatua zinazostahili. *(Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mauaji ya mifugo katika ameneo hayo yamekuwa yenye kujirudia mara kwa mara. Kwa mfano kati ya mwaka 2009 na sasa zaidi ya ng'ombe 200 wameuawa katika maeneo hayo ikiwa pamoja na matukio ya hivi karibuni ambayo yaliyofanyika katika Kijiji cha Ikuba pembezno mwa Mto Ikuba ambao maji ya Mto huo yanategemewa na wanakijiji, mifugo pamoja na wanyamapori. Ushahidi wa kutosheleza wa jambo hili upo:-

(a) Je, Wizara yako, Mheshimiwa Waziri utakapoletewa ushahidi wa kutosheleza juu ya tukio hili, utachukua hatua gani na utakuwa tayari kuwalipa wafugaji hao fidia zao?

(b) Mnamo tarehe 30, Aprili, 2009 Serikali ilitoa kauli, kauli ya Serikali iliyotolewa na aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Celina Kombani kuhusu kadhia ya wakulima na wafugaji na uporaji wa ng'ombe uliofanywa kwa wafugaji katika Mikoa ya Rukwa, Tabora na Morogoro na ikasitisha zoezi hilo na Serikali ikaunda Tume ili kufuatilia jambo hilo mpaka sasa toka 2009 hakuna fidia zilizolipwa kwa wale

walioathirika kwa zoezi hilo ambalo lilikuwa la uporaji na wala Serikali haijatoa taarifa nyingine yeyote ndani ya Bunge hili. Sasa Mheshimiwa Waziri, una maelezo gani juu ya hilo?(*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi kwamba katika mazingira ambayo tunayo hivi sasa wahalifu wameongezeka na hakuna ushahidi wa moja kwa moja unaodhibitisha kwamba ni askari wa wanyamapori wanafanya hivyo na niseme tu kwamba matukio haya ambayo yanatokea kwa wananchi, yanatokea.

Vile vile kwa askari kwa masikitiko nilifahamishe tu Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi cha miaka minne iliyopita Wizara au Serikali imepoteza watumishi wake wanane (8) kwa kuuwawa na majangili, kwa risasi kwenye maeneo ya Hifadhi wakifanya kazi. Katika matukio yote haya, wale ambao wanapambana nao wanakuwa na silaha nzito za kivita.

Kwa hiyo, katika mazingira haya si rahisi kuweza kudhibitisha moja kwa moja kwamba askari wetu ndiyo wanaofanya hayo kwa sababu mhalifu anaweza akajika- *maflage*, akaweza kuvaa nguo za askari na akapora mifugo ya watu wengine. Wakati huo wakimwona wanadhani kwamba ni askari wa kwetu wa Hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kama nilivyosema mwanzo kwamba masuala haya ni ya kijinai na katika kila eneo kuna vyombo vya ulinzi na usalama. Kwenye Wilaya, Mkuu wa Wilaya ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na Polisi ndiyo chombo au mamlaka ambayo imepewa dhamana ya kulinda maisha ya wananchi na mali zao.

Matukio kama haya ni vizuri yanapotokea mara moja yanaripotiwa polisi kwa sababu ni ya kijinai na wala sio ya kiuhifadhi *as such*. Kwa hiyo, yanapotokea yanaripotiwa polisi na polisi wanaweza kuchukua hatua na askari wetu hawaruhusiwi kufanya hayo yanayoelezwa kwamba yanafanyika.

Kwa maana hiyo inapotokea kwamba askari wetu wa Hifadhi wamefanya, wanakuwa ni wahalifu kama mhalifu mwingine yeyote na sheria inachukua mkondo wake. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili la Mifugo ambayo ilikuwa inaondolewa kwenye maeneo niseme suala hili kama ambavyo lilikwisha kuelezwa hapo kabla lilikuwa linasimamiwa na Serikali na taarifa zilikuwa pia zingeweza kutolewa na Wizara husika ya Mifugo. Kwa hiyo, kwa sisi kwa upande wetu kama Wizara siwezi nikasema kwamba ni fidia kiasi gani na italipwa lini kwa wananchi walioathirika na zoezi hilo. Ila niombe tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu tusaidiane kwamba sasa hivi uvamizi wa mifugo kwenye maeneo yaliyofadhiwa ni mkubwa sana kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na kutokana na uharibifu wa mazingira kwenye maeneo yasiyohifadhiwa. Kwa hiyo, tuombe kwamba wananchi waliovamia kwenye maeneo yaliyohifadhiwa ni vizuri wakaondoka ili kuepusha migongano ambayo sio ya lazima kati ya Serikali na wananchi wake.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pori la hifadhi la Luwanfi tulilikabidhi kwa Serikali Kuu kwa mapatano kwamba baada ya kukabidhiwa tutaweka mipaka upya ili wananchi wa Nkansi wafaidike wapate baadhi ya sehemu kwa ajili ya kilimo.

Je, Wizara yako lini itaweka mipaka upya kwa hiyo *game reserve* ya Lwafi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kessy, Mbunge wa Nkasi, kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Pori hili la Lwafi, Wizara yangu ilishakubali kulisimamia kwa maombi ya Halmashauri na toka mwezi Julai mwaka 2011 Wizara imekuwa ikifanya doria kwenye maeneo hayo na kwa kushirikiana na Halmashauri, zoezi la uhakiki wa mipaka linaendelea na ninashukuru sana kwa eneo hili tunashirikiana vizuri sana na wananchi pamoja na Halmashauri, nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaongeza kasi ya kuhakikisha zoezi hili linakamilika mapema.

**MHE. JOHN M. CHEYO**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa askari wa pori ambalo liko katika sehemu ya Lungwa, Ngwalali, Ngwamtani, Shishani na Longalombogo na Nkuyu askari wako sasa wanafanya biashara ya kukamata ng'ombe, wanawapeleka porini, wanawaweka kwenye zizi, wanaanza kuchukua milioni 5 kila wiki kutoka kwa wafugaji hawa, wakimaliza wiki hii Ngwalali wanahamia Longalombogo, wakimalimaza Longalombogo wanahamia Nkuyu, wakimaliza huku, hii biashara haramu Mheshimiwa Waziri unasemaje, unatamka nini juu ya kumaliza tatizo hili? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili analozungumzia Mheshimiwa Mbunge lina matatizo ya ukweli kwamba wananchi hawana eneo la kulisha mifugo yao, pale Wizarani waliwahi kuja uongozi wa wafugaji kutoka Bariadi, walikuja kuniomba kwamba tunaomba Mheshimiwa Waziri utueleze faini ya mwaka mzima ni kiasi gani ili tulipe tuweze kulisha mifugo yetu mwaka mzima. Kwa sababu haiwezekani tusiingize mifugo yetu hifadhini kwa sababu hatuna kabisa ardhi.

Kwa maana hiyo suala la kuigiza mifugo tukapigwa faini kwetu sisi ni la kawaida. Kwa hiyo, sidhani kwamba ni kweli kwamba askari wanakwenda kuchukua mifugo kwenye Vijiji kuingiza hifadhini, isipokuwa kwa sababu hakuna kabisa malisho imekuwa sasa ni *practice* kwamba kila siku mifugo inaingizwa mle na kila siku faini inatozwa.

Pili ni hili suala la faini kutozwa kutokufuata utaratibu na wakati mwingine fedha hizo kutokufika Serikalini. Nimekwishakusema mara kadhaa kwamba wananchi wasikubali kutozwa faini bila kuridhia kwa sababu kimsingi mwananchi au mhalifu anatozwa faini baada ya yeye kuridhia ku-*compound* ile *offence*. Asipokubali kesi inapelekwa mahakamani na pale anapokubali ku-*compound* ile *offence* inabidi alipe ile faini ambayo inakuwa imewekwa kisheria na apewe stakabadhi.

Kwa hiyo, nisisitize tu kwamba matukio ambayo yanatokea ya wananchi kutozwa na kutokupewa risiti ni makosa na wananchi wasikubali kufanyiwa hivyo. Lakini pia tutafute *solution* ya kudumu ya tatizo la malisho kwa maeneo hayo.

Na. 85

**Mifugo Kutoka Nchi Jirani Kuchungwa Kwenye Mkoa wa Kagera**

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE** aliuliza:-

Serikali ilipojibu swali Na. 90 lililoulizwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, kuhusu wanyama waharibifu hasa tembo ilikiri kuwepo kwa mifugo mingi kutoka nchi jirani inayochungwa katika eneo la Kagera:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuwaondoa wavamizi hao na mifugo yao ambayo imeleta madhara makubwa kiuchumi, kijamii na hata kuharibu mazingira?

(b) Je, Serikali iko tayari kuunda tume kuchunguza tuhuma za mauaji na rushwa kwa watendaji wa Serikali ambao wameshindwa kutimiza wajibu wao wa kuwalinda wananchi na maeneo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kasikazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wilaya za Mkoa wa Kagera zina changamoto ya kukabiliana na wafugaji haramu kutoka nchi jirani hususan wakati wa kiangaza. Hii inatokana na historia, mahusiano ya kijadi na ya kijamii baina ya wananchi na wenzao wa nchi jirani na kuwepo kwa mapori makubwa yenye malisho mazuri kama vile pori la Ibanda, Burigi, Biharamulo, Kitengule na Kimisi.

Taarifa za Mkoa zinaonyesha kuwa mapori haya huweza kuwa na wafugaji haramu takriban 1,000 na ng'ombe zaidi ya 120,000. Wingi huu wa mifugo na wafugaji haramu husababisha athari za kijamii na mazingira kwa nyakati na viwango tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na madhara hayo Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya doria, kuelimisha na kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kutoa taarifa kuhusu wavamizi, viongozi na tume mbalimbali kukutana na wananchi, kuwa na mikutano ya ujirani mwema na nchi husika na kukamata, kutoza faini na kurudisha wafugaji haramu na mifugo yao walikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwezi Agosti, 2006 na Mei, 2007, Serikali ilifanya operesheni iliyowezesha kukamatwa kwa ng'ombe 13,986 na kurudishwa Uganda. Aidha, katika kipindi hicho hicho walikamatwa ng'ombe wengine 9,772 na kurudishwa Rwanda. Mwezi April, 2012 walikamatwa ng'ombe 600 katika ranchi za *NARCO* Wilayani Misenyi na kutozwa faini ya sh. 50,000 kwa kila ng'ombe na hivyo jumla ya sh. 30, 000,000 zilikusanywa. Katika operesheni iliyofanyika mwaka 2011 hii iliwezesha jumla ya wavamizi 43 kukamatwa wakiwa na ng'ombe 2,140 na hawa walirudishwa Rwanda. Serikali itaendelea na juhudi hizi ili kukomesha uvamizi huu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la mauaji na rushwa kwa watendaji wa Serikali lipo nje ya majukumu ya Wizara yangu, naomba kwa kuwa Serikali yetu ni sikivu, mamlaka husika zitachukua hatua zinazostahili ikiwa ni pamoja na kuunda tume ikionekana inahitajika kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nasikitika kwa majibu ya Serikali yangu kukiri udhaifu. Maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa taarifa za uhakika kutoka Mkoani Kagera ambako mimi nawakilisha ng'ombe ambao aliwaona Waziri wa Mamabo ya Ndani bado wapo na hakuna ng'ombe walioondoka. Serikali yangu inawaahidi nini tena wananchi wa Kagera kwamba wale ng'ombe ambao wapo sehemu za Kimisi, Muleba, Misenyi, Serikali itakwenda kuwaondoa sasa? ( *Makofi*)

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Mifugo, Maji na Kilimo ilikwenda katika eneo langu Jimbo la Muleba Kaskazini, Lutoro uonevu ninalolizungumza kuhusu wananchi wangu, Kamati ya Bunge iliuona, wananchi walikiri kwamba akina mama wanakabwa, walikiri kuwepo wageni kutoka nchi za nje. Kuna taarifa kutoka kwa *OCS* wa Kishuro kwamba watu wanatumia silaha na kuwateka watu. *(Makofi)*

Swali langu, kwa kuwa sasa Serikali imekiri madhaifu hamwoni sasa mliombe Bunge iunde Tume teule kwa kasi ile ile ya kasi ya gesi na mali asilia zilivyosimamiwa basi Bunge lisimamie suala la Lutoro na Mkoa wa Kagera kwa ujumla? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli kama anavyosema mwaka jana nilifanya ziara mahususi katika Mkoa wa Kagera ili kuangalia tatizo la uhamiaji haramu pamoja na wafugaji wanaotoka katika nchi jirani hasa nchi ya Rwanda.

Katika ziara ile nilikutana na Kamati za Ulinzi na Usalama katika ngazi ya Wilaya na ngazi ya Mkoa na niliwaelekeza kwamba kuna haja sasa ya Serikali kuanza kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba wahamiaji wote haramu pamoja na wenye mifugo wanaotoka nchi jirani warudi makwao na Kamati za Ulinzi na Usalama zilinihakikishia kwamba zitachukua hatua hiyo inayo stahiki.

Nimeahidi pia kwamba katika siku za hivi karibuni nitarudi tena ili kuangalia utekelezaji. Sasa jambo la kusikitisha ni kwamba Mheshimiwa Mbunge anasema bado ng'ombe wapo lakini kwa bahati mbaya sijapata taarifa hizo na kwa kuwa namsikia yeye basi ile ziara ambayo nimekusudia kuipanga hivi karibuni nitafanya kila linalowezekana kwamba nifanye ziara hiyo haraka ili Serikali ichukue hatua zinazostahiki.

Lakini kwa kupitia Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wa Mkoa wa Kagera nawaomba sana kwamba kunapokuwa na taarifa za vitendo vya uvunjifu wa amani tupeane taarifa mapema. Lakini lazima tukiri kwamba wanaofanya vitendo hivi wengine ni wananchi wanaowaficha hawa wahamiaji

haramu. Sasa ni vizuri kwamba wakati wa kufanya muhali uwe umekwisha sasa, taarifa zinapopatikana zitolewe mapema. *(Makofi)*

Ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Wabunge wengine wa Mkoa wa Kagera na maeneo mengine ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara yangu haitasita, itachukua hatua kama inavyostahiki. Naomba watuamini, tutafanya kazi hiyo kwa uaminifu mkubwa na kwa uadilifu, kwa maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Swali la pili, suala la kwamba kuna akina mama wanabakwa, hivi Waheshimiwa Wabunge tunangoja muda wote akina mama, wake zetu na watoto wetu wanabakwa halafu tunasubiri kuja kutoa taarifa huku Bungeni, mbona tumechelewa sana! Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, taarifa hiyo nimeisikia, nitashirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama na kuvielekeza kwamba, tuchukue hatua zinazostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Swali hili kwa umuhimu wake, naona bado Wabunge wa Kagera wamesimama, nimpe nafasi Mheshimiwa Blandes, aulize swali fupi sana la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, naishukuru Serikali, mwaka 2006 nilileta tatizo hili Bungeni, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa akiwa Waziri wa Mifugo na Mheshimiwa Edward Lowassa akiwa Waziri Mkuu, walijitahidi sana kulishughulikia suala hili kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya zoezi lile la mwaka 2006 tatizo hili tumekuwa tukilitolea taarifa hapa Bungeni na tatizo hili siyo la Mkoa wa Kagera ni la usalama wa nchi yetu ya Tanzania. Nchi yetu sasa hivi imevamiwa na wageni kutoka Rwanda na Burundi. Nasikitika sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, amesimama na kutoa majibu mepesi sana kama vile jambo hili ni la kawaida anasema taarifa haziji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wa Mkoa wa Kagera Bunge lililopita tuliiandikia Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani tumempa barua, Mheshimiwa Waziri Mkuu tumempa barua, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo amepewa barua, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi amepewa barua ...

**NAIBU SPIKA:** Sasa swali Mheshimiwa.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata uchungu mkubwa sana kuona Serikali inakaa inasinzia, inashindwa kutimiza wajibu wake wa Kikatiba wa kulinda nchi pamoja na mali zake. Nilikuwa naomba niulize ni lini; hatutaki ziara za Waziri; lini Serikali itawaondoa wahamiaji haramu na mifugo yao kurudi kwao? Hili zoezi liwe la moja kwa moja la kudumu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Serikali inasinzia.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie Serikali hii haisinzii, ndiyo maana Mheshimiwa Mbunge anathubutu kusema hayo anayoyasema kwa sababu Serikali hii inafanya kazi. Naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, anasema kwamba suala hili tusilishughulikie kwa kufanya ziara. Amesema hapa suala hili linahusu amani na usalama wa watu wake. Sasa kwa kuwa mimi ndiyo msimamizi mkuu wa masuala ya ulinzi na usalama; kwa nini nisifanye ziara ili kuhakikisha kama watendaji wangu wanatekeleza wajibu wao?

Narudia tena, nahisi kwamba ni uamuzi sahihi mimi kufanya ziara huko ili nione kile kinachotokea na baada ya kumaliza Bunge namhakikia Mheshimiwa Mbunge kwamba, nitafanya ziara katika eneo linalohusika, tukae, tuwasimamie wanaohusika na mara moja tuwahamishe wale ambao wanaleta mifugo kutoka nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Na. 86

**Hitaji la Kituo cha Polisi Ukonga**

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA** aliuliza:-

Jimbo la Ukonga lina wakazi zaidi ya 323,000, idai ambayo inaongezeka kwa kasi na vitendo vya uhalifu vimezidi kuongezeka hasa katika Kata za Chanika, Majohe, Msongola, Kivuke na Kitunda:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo kikubwa cha Polisi katika Jimbo hilo kukabiliana na vitendo vya uhalifu vinavyoonekana kukithiri kwenye maeneo hayo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati mwafaka kuvikarabati na kuvipanua vituo vidogo vilivyopo, vinavyoonekana kuchakaa sana katika Kata za Ukonga, Gongolamboto, Pugu na Chanika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eugen Elishiringa Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ukonga lipo katika Wilaya ya Kipolisi ya Ukonga na tayari kipo Kituo kikubwa cha Stakishari ambacho kina hadhi ya Wilaya. Hata hivyo, wazo la Mheshimiwa Mbunge la kujenga kituo kingine kikubwa katika Jimbo hilo ni jema na tayari tumeshaanza kushirikiana naye ili kutimiza azma hiyo. Tunamshukuru kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika eneo hilo. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hali ya usalama wa raia na mali zao katika Kata alizozitaja siyo mbaya kutokana na juhudi zinazofanywa na Polisi kwa kutumia dhana ya Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mpango wa kujenga na kukarabati vituo vya polisi na nyumba za kuishi askari nchi nzima. Hata hivyo, kama ambavyo nimekuwa nikieleza katika Bunge hili, nia hii njema inakwamishwa na upungufu wa rasilimali fedha.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kuwepo na upungufu mkubwa wa rasilimali fedha; na kwa kuwa Wananchi wa baadhi ya Kata katika Jimbo la Ukonga kwa nguvu zao wenyewe wameweza kujenga vituo vya polisi kama walivyofanya katika sehemu ya Mvuti na Msongola kwa miaka mingi sasa; na kwa kuwa Serikali imeshindwa kuwapatia askari polisi katika vituo hivyo kwa kisingizio cha kuwa sehemu hiyo ni mbali. Je, Serikali inasema nini sasa kuhusu jukumu la askari wa kuwalinda Wananchi wa Tanzania na mali zao?

Pili, kwa kuwa ulinzi shirikishi katika Jimbo la Ukonga kama alivyokiri Mheshimiwa Waziri umekuwa msaada mkubwa sana kwa Serikali na jamii nzima; na kwa kuwa sasa vikundi vingi vya polisi vya ulinzi shirikishi vina changamoto kubwa sana ya kutokuwa na vifaa kama vile simu, usafiri, nguo na kadhalika. Je, Serikali inasema nini sasa katika kuvisaidia vikundi hivi kupata vifaa hivyo ili waweze kufanya kazi zao kikamilifu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyojibu katika swali lake la msingi ni kwamba, kila jitihada zinafanyika na juhudi zinafanyika kuhakikisha kwamba, askari au jeshi la polisi linasimamia ulinzi wa raia na mali zao. Hapo hapo tumekuwa tukisema katika Bunge hili Tukufu kwamba, tatizo ambalo limekuwa likitukwaza katika kutimiza malengo yetu katika kuhakikisha kwamba yote ambayo tumeyawekea azma yatekelezwe limekuwa ni suala la rasilimali fedha. Naomba nimhakikishie kwamba, sisi kama Wizara na Jeshi la Polisi, tunashukuru kwa jitihada ambazo zinafanywa na Wananchi katika kuweka nguvu zao kujenga vituo kadhaa.

Hii siyo katika eneo hili la Mheshimniwa Mbunge, lakini katika maeneo mengi tu katika Tanzania, ambayo Waheshimiwa Wabunge hapa mnatoka na naomba niwashukuru kwa jitihada ambazo mnazifanya.

Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba, hili suala alilolisema kwamba polisi hawakupatikana tutazungumza hawakupatikana kwa namna gani, maana amesema kwamba alileta hili lakini kulikuwa polisi hawakupatikana. Ningeomba tulizungumze lipatiwe ufafanuzi tuone hawakupatikana kwa namna gani na kama kuna njia za kutatua hilo tuweze kutatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili linahusu Kituo cha Stakishari, kama alivyosema kwamba, ulinzi shirikishi imekuwa ni jambo kubwa sana na linasaidia. Kama anavyosema, kumekuwa na upungufu wa vifaa, nguo na kadhalika, ama tuseme sare za polisi na kadhalika, hii ni kwamba tunakiri, lakini jitihada zinafanyika na tatizo ambalo linatukwaza katika maeneo yote haya ni rasilimali fedha na laiti kama bajeti ingekuwa inaruhusu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, tungefanya kazi iliyokuwa bora zaidi.

Na. 87

**Hali Mbaya ya Hosteli za Wanafunzi wa Taasisi ya Sayansi Baharini – Zanzibar**

**MHE. WARIDE BAKARI JABU** alijibu:-

Taasisi ya Sayansi Baharini - Zanzibar *(Institute of Marine Science -Zanzibar (IMS))* inazo nyumba mbili kwa ajili ya hosteli za kulala wanafunzi wake; lakini nyumba hizo zimeharibika vibaya ikiwemo moja kuungua moto na nyingine kuwa na nyufa kubwa licha ya suala hilo kuripotiwa sehemu zinazohusika.

(a) Je, kwa nini mpaka sasa Serikali haikuipa hosteli hiyo kipaumbele kwa kutenga bajeti ya ukarabati wa hosteli hizo kwa mwaka 2011/2012?

(b) Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa wa majengo hayo ili yaweze kutumiwa na wanafunzi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembesamaki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba mbili zilizoainishwa na Mheshimiwa Mbunge sio hosteli za wanafunzi bali ni nyumba za wafanyakazi wa Taasisi hiyo ya *IMS* (*Institute of Marine Science)*. Nyumba hizi ziligeuzwa kuwa makazi ya muda kwa wanataaluma wa nje wanaokuja kufanya utafiti wa sayansi na bahari katika taasisi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hosteli za kudumu za wanafunzi zinatarajiwa kujengwa eneo la Buyu katika awamu ya mwisho ya ujenzi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari. Ujenzi unaoendelea sasa pale ni kwa ajili ya madarasa, ofisi pamoja na maeneo ya kufanyia tafiti (Sehemu A na B) ambao utagharimu kiasi cha shilingi bilioni 4.3. Fedha hizo tayari zimekwishatengwa kwa kazi hiyo. Kwa sasa wanafunzi wa *IMS* (*Institute of Marine Science),* wanaishi katika nyumba walizopangiwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika maeneo mbalimbali mjini Unguja.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri, naomba kumwuliza Naibu Waziri maswali mawili. Kwanza, napenda kuishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho. Lakini napenda kumwuliza swali langu la msingi lilikuwa je, kwa nini ukarabati wa hizo nyumba haujatengewa fedha. Kwa hiyo, nataka kujua ni lini ukarabati huo utafanyika?

Pili, napenda kumwuliza kwa kuwa ametueleza kuwa kwa sasa hivi wanafunzi wa kutoka Taasisi ya Sayansi Baharini wamepangiwa nyumba katika sehemu mbalimbali na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mjini Unguja. Je, ni lini hosteli za wanafunzi hawa zitamalizika kujengwa? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi kwamba, Serikali ilitenga bilioni 4.3 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na ofisi na sehemu zingine za utafiti katika chuo hiki. Lakini kwa mwaka huu wa fedha kwa sababu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndiyo msimamizi na ni kama ni tawi la pale wametenga jumla ya bilioni 3.5 kwa ajili ya kuendelea kumalizia ujenzi na fedha zimeshapelekwa na ujenzi mpaka sasa hivi ninavyosema unaendelea.

Lingine ni kwamba ni lini sasa? *BOQ* inaonesha tarehe ya kumalizika kwa ujenzi huu ni mwezi Juni, mwaka huu 2012.

Na. 88

**Wananchi Kupimiwa Maeneo ya Malisho**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA (K.n.y. MHE. MICHAEL L. LAIZER)** aliuliza:-

Wananchi wa Longido wanazingatia matumizi bora ya ardhi na wameshatenga maeneo ya malisho katika kila Kijiji na Kata:-

Je, Serikali itawapimia lini wananchi hao maeneo ya malisho ili waondokane na migogoro kati ya wafugaji na wakulima?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Michael Lekule Laizer kwa namna anavyofuatilia kwa karibu maendeleo ya wananchi wa Jimbo lake. Pili, nawapongeza wananchi wa Jimbo la Longido kwa kushiriki katika kutenga matumizi ya ardhi katika kila Kata na Kijiji kwa utaratibu wa mipango shirikishi. Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi, iliiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Longido kwa kuunda Timu ya Usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya yaani *Participatory Land Use Management (PLUM)* ambayo kwa pamoja waliandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji vya Eworenedeke na Kimokoa. Lengo lilikuwa kuiwezesha Timu ya *PLUM* kuendelea kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji vingine, Wilayani Longido.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Longido kama Mamlaka ya upangaji mipango ya matumizi bora ya ardhi kuiwezesha timu ya *PLUM* kuendeleza zoezi la kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Vijiji, Wilayani humo.

Baada ya hatua ya kupanga matumizi ya ardhi kukamilika, hatua inayofuata huwa ni kujenga masjala za ardhi ya kijiji kwa ajili ya kuhifadhi vyeti vya ardhi vya vijijii na nyaraka nyingine kama hatimiliki za kimila.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu inakamilisha utayarishaji wa programu ya Kitaifa ya kupima mashamba ya wanavijiji na kutoa hatimiliki za kimila kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana kutoka kwenye Wilaya za majaribio zikiwemo Babati, Iringa Vijijini, Mbozi, Bariadi, Manyoni na Namtumbo. Programu hii itatekelezwa kwa kuwashirikisha wafadhili kama Benki ya Dunia na Sekta Binafsi kuanzia mwaka 2012/2013. Kwa sasa hali halisi ya bajeti ya Wizara ya Ardhi hairuhusu upimaji wa maeneo yote nchini kulingana na mahitaji. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Longido inahimizwa itenge fedha na inaweza kushirikiana na sekta binafsi kuanza kupima mashamba hayo kwa awamu, kama ilivyofanyika kwa Wilaya ya Hanang ambapo mashamba ya wananchi yamepimwa na Hatimiliki za kimila zinaendelea kutolewa mwaka huu kwa juhudi zao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuzielekeza Halmashauri za Miji na Wilaya kufanya maandalizi ya kutekeleza Programu ya Kitaifa ya kupima mashamba na kutoa Hatimiliki za kimila. Pia, ni muhimu watenge fedha kwa ajili ya utekelezaji kupitia bajeti zao maana hali halisi ni kwamba, bajeti ya Taifa haikidhi mahitaji yote.

Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na kukubaliana kwamba bajeti ya Wizara ya Ardhi ina ukomo katika kukidhi upimaji wa vijiji vyote vya nchi hii, lakini kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Longido wakiongozwa na Mbunge wao na Madiwani walizunguka vijiji vyote vya Halmashauri ya Wilaya ya Longido na kuhamasisha wananchi kupanga matumizi bora ya ardhi na wananchi wakaitikia na kutenga maeneo ya mifugo na maeneo ya kilimo. Je, Waziri anatuambiaje katika ushauri ninaoutoa kwa kuishauri Serikali itenge fedha kwa awamu ili kuunga mkono jitihada hizi za wananchi za kutenga maeneo haya ili kuepusha vurugu au mgogoro kati ya wafugaji na wakulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali dogo la pili, Wilaya ya Longido imekumbwa na ukame katika miaka ya karibuni na kuwaacha wafugaji wa Wilaya ya Longido katika umaskini uliotopea na hivyo kuwafanya kukosa uwezo wa kupima maeneo hayo kwa uwezo wao wenyewe. Je, Serikali inaonaje kutenga fedha kwa ajili ya kusaidia Wilaya ya Longido katika upimaji wa vijiji hivi na kuweka mipango hii bora ya ardhi kama ilivyoamua kutenga fedha kwa ajili ya kuwanunulia mifugo wafuaji hawa ambao wameachwa katika umaskini uliotopea?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa nataka niwape pole wananchi wa Longido waliokumbwa na ukame. Kama maafa mengi na ukame unawasukuma wananchi katika hali ya umasikini, nataka tu nimwahidi Mheshimiwa Ole-Sendeka na Mheshimiwa Laizer, kwa kufikisha ujumbe wangu kwa wananchi kwa ujumla kwamba, tatizo hili tunaliangalia. Lakini Wizara ya ardhi yenyewe inafanya kazi kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla, katika suala hili la kutafuta fedha za kutosha kupima mashamba, suala hili ni lazima lipewe kipaumbele katika ngazi ya Halmashauri. Kwa upande wangu mimi ninafahamu kwamba, Wizara yangu ilipewa ruhusa ya kubaki na chochote tutakachokusanya. Niahidi tu kwamba, katika kila Sh.100/= ambayo Wizara ya Ardhi inakusanya, Sh. 30/= zibaki hapo hapo kwenye Halmshauri kusudi zisaidie mipango kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala kwamba Longido tayari walishahamasisha, nimekiri kwamba Tume yetu ya Matumizi Bora ya Ardhi kweli imefanya kazi hii, lakini huwa ninapenda kusema mambo kama yalivyo; kwa sasa hivi, bajeti ya Serikali mambo yanavyokwenda, tutajitahidi katika kipindi kijacho. Lakini itategemea ninyi Waheshimiwa Wabunge, kama *appropriators* kutuangalia kwa jicho la huruma. Nashukuru.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Hivi karibuni tumepitisha azimio la kuridhia Mkataba wa Vijana Afrika, na moja ya ibara katika Mkataba huo inahusu nchi wanachama kuwawezesha vijana kumiliki ardhi ili kujiondoa na umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa kujua, Wizara husika ina mkakati gani au imejipanga vipi; si kimaandishi, si kimaneno, kuhakikisha vijana wa Tanzania wananufaika na ardhi yao; iwe wafugaji, iwe wakulima na hata wenye uwezo wa kumiliki ardhi kwa ajili ya kujenga nyumba? Nilikuwa naomba kupata majibu sahihi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba, suala la vijana kupata ardhi hata na mimi ni kitu ambacho wala hakina mjadala. Ni kitu ambacho tunatakiwa tukifanyie kazi kwa pamoja na inapokuja vijana kupata ardhi za kujenga nyumba mijini, huwa ninataka nitoe rai na wito kwa vijana kwamba, wasibaki nyuma, walete maombi. Kwa sababu, ardhi za mijini zinatolewa kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya Ardhi na pia Mipango Miji. Kwa hiyo, vijana wanaweza hata wakajiunga kwa vikundi kusudi wawe na nguvu zaidi kuweza kujenga nyumba. Maana itakuwa ni jambo la kusikitisha vijana wakipewa viwanja halafu wakashidwa kujenga, miaka mitatu tukarudi kuwapokonya. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba, suala la kuwapatia vijana ardhi mijini ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapo hapo niongezee pia, vijana walio wengi vijijini tuna taarifa kwamba wengine hawana ardhi za kilimo, na suala hili Serikali inalitambua. Wakati wa bajeti, niliongelea kwa kirefu kwamba, wale ambao wana mashamba makubwa na hawayatumii na wameishia

kuwakodisha vijana, siku zao zinahesabiwa. Tuko katika sensa, tutaweza kuchukua mashamba yale kusudi tuwagawie vijana. Nakushukuru. *(Makofi)*

Na. 89

**Ujenzi wa Mifereji – Bungoni**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU** aliuliza:-

Wananchi wa Bungoni walio karibu na mfereji wa Bungoni, kupitia daraja la Malapa wamekuwa wakikumbwa na mafuriko ya mara kwa mara hasa nyakati za mvua. Ili kuweza kujenga miundombinu ya mifereji hiyo, itahitajika Sh. 2,300,000,000/= kazi ambayo imeshaanza.

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba, ujenzi huo unakamilika kwa muda uliopangwa ili kuondoa kero hiyo inayowapata wananchi?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mfereji wa Bungoni unatekelezwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara nchini *(TANROADS)* katika Mkoa wa Dar-es-Salaam. Ujenzi huo unahusisha ujenzi wa mfereji mkubwa wa urefu wa meta 860, ujenzi wa madaraja mawili kwa ajili ya magari kupita juu ya mfereji, ujenzi wa madaraja manne kwa ajili ya watembea kwa miguu kupita juu ya mfereji, ujenzi wa makalvati katika Barabara ya Uhuru na katika njia ya reli pamoja na ujenzi wa kalvati kubwa lenye urefu wa meta 282 kuanzia njia ya reli hadi Barabara ya Nyerere eneo la Mtava.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu, ulianza tarehe 22 Novemba, 2009 kwa gharama ya Sh. 2,180,775,000/=. Kazi za ujenzi zinaendelea vizuri ambapo ujenzi umefikia asilimia 75 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu wa Februari, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba baada ya kukamilika kwa mradi huu, mafuriko ya mara kwa mara yaliyokuwa yanawakumba wananchi wa Bungoni yatapungua kwa kiasi kikubwa. Aidha, napenda kutoa wito kwa wananchi waishio kando kando ya mfereji huo, kuutunza kwa kutotupa taka na kutoelekeza maji taka katika mfereji huo.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatana na mimi kwenye mfereji huo na yeye akaridhika kiwango hicho alichokitaja hapa kuwa kimekamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mfereji huu unaanzia barabara ya Nyerere na umepangiwa pesa mpaka daraja la Malapa, Barabara ya Uhuru. Lakini baada ya Barabara ya Uhuru kuelekea mto wa Msimbazi maeneo ya Sharifshamba, hakuna mpango wowote wa kuendeleza mfereji huu. Je, Serikali haioni sasa mafuriko yanahama kutoka Bungoni na yatakwenda kuhamia Sharifushamba?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zungu. Kulikuwa na nyongeza ya Mheshimiwa Rage kwamba mafuriko yale ya mabondeni, kuna baadhi ya watu pale Jangwani, mbona hawahami? Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Zungu, sina tatizo kutembelea na yeye huko ili twende tukakague mara muda utakapofika. Nami nafikiri hicho ni kitu kizuri tu wala sina tatizo nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu utekelezaji wa mradi huu, nimeeleza kwamba, kalvati zenye ukubwa wa meta mbili kwa meta kumi katika Barabara ya Uhuru umekamilika. Mfereji wa wazi wenye

upana wa wastani wa meta 1.6 na wastani wa kina cha meta 1.5 na urefu wa meta 860 nao umekamilika. Madaraja mawili kwa ajili ya magari kupita juu ya mfereji yamekamilika. Lakini pia kalvati lenye ukubwa wa meta 1.2 kwa meta 2.5 kwa meta 15 lenye urefu katika njia za reli, nao umekamilika. Kalvati lenye urefu wa ukubwa wa meta mbili kwa meta nne, na urefu wa meta 282 nao umekamilika. Katika eneo lingine ambalo amelizungumza Mheshimiwa, tutaendelea kuliangalia ni kwa namna gani tunaweza tukaliendeleza mara baada ya sehemu hii ya kwanza kukamilika kutenegenzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wito wangu, napenda kusisitiza kwamba wananchi wa maeneo hayo panapopita huo mfereji, wasitupe takataka kwenye mfereji huo kwa sababu, utaziba tena na mafuriko yatawapeleka. Kwa hiyo, wahakikishe wanautunza, takataka zisimwagwe mle ili kurahisisha upitaji wa maji yanayotoka katika maeneo ambayo yanakumbwa na mafuriko.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri, yanaonyesha kwamba huu mfereji wa Bungoni umeanza kujengwa kuanzia mwaka 2009, na huu ni mwaka wa 2012, bado kazi haijakamilika. Naelewa kwamba, changamoto kubwa inayoikabili *TANROADS* Mkoa wa Dara-es-Salaam ni uhaba wa rasilimali za kukamilisha miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kuwa mifereji mingi, madaraja pamoja na kalvati kwenye barabara zinazohudumiwa na *TANROADS* Mkoa wa Dar-es-Salaam inasuasua kujengwa kutokana na ufinyu wa rasilimali kwa upande wa *TANROADS:* Je, Wizara imefikia wapi katika kushughulikia mapendekezo ya Mkoa wa Dar-es-Salaam toka miaka kadhaa nyuma ya kupandisha hadhi barabara hizi za Dar-es-Salaam ili Serikali iweze kuongeza nguvu za ziada za kifedha kwa kuwa barabara zitakuwa zinahudumiwa moja kwa moja na *TANROADS?*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba Mkataba wa utengenezaji wa mfereji huu ulianza mwaka 2009 na katika siku za nyuma kidogo fedha hazikuweza kupatikana. Ni kwa sasa hivi fedha zimepatikana za kutosha. Hadi sasa Mkandarasi huyu ambaye anaitwa *Africo Engineering & Construction Co. Limited* wa Dar-es-Salaam amekwishalipwa Sh. 1,398,814,551/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ombi la Mkoa wa Dar-es-Salaam la kupandisha hadhi baadhi ya barabara ambazo zinatakiwa zihudumiwe moja kwa moja na *TANROADS,* nimepata barua hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa. Wameleta maombi ya barabara kati ya 27 hivi, ambazo zinatakiwa kupandishwa hadhi. *Consultant* wa Wizara na Wataalamu wanazipitia ili kuona kama kweli barabara hizo zitastahili kupandishwa; na zikishapandishwa, nitatoa taarifa ili ziweze kuhudumiwa na *TANROADS* moja kwa moja Mkoa wa Dar-es-Salaam, ambapo Mkoa wa Dar-es-Salaam unahudumia kilometa 560 ya barabaraba zilizo chini ya *TANROADS.* Kwa njia hiyo, zitaweza kupatikana fedha za kutosha katika kuhakikisha barabara za Dar-es-Salaam, zinatengenezwa.

Na. 90

**Kung'olewa kwa Injini ya Kivuko Kipya cha Mto Ruhuhu**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Miaka miwili iliyopita, Serikali ilinunua kivuko kipya na kukiweka kwenye mto Ruhuhu ili kuondoa tatizo la usafiri kwa watu wa Ruvuma na Iringa:-

(a) Je, kwa nini Serikali imeng'oa injini yake na kwenda kuifunga kwenye kivuko cha mto Kilombero?

(b) Je, Serikali haioni imewadharau na kuwabagua kwa hali ya juu wananchi waliokuwa wamepewa kivuko hicho?

(c) Je, kwa kitendo hicho, Serikali inataka kuwaambia Watanzania kuwa kuna wananchi wa daraja la juu na wengine wa daraja la chini ambao hawana haki ya kupata huduma katika nchi yao?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi Agosti, 2011, injini moja ya kivuko cha Kilombero iliharibika kwa kiwango cha kutotengenezeka hivyo kusitisha mawasiliano kati ya Wilaya ya Kilombero na Ulanga Mkoani Morogoro. Wakati huo kivuko cha mto Ruhuhu kilikuwa kimesimamishwa kutokana na kina cha maji kupungua sana. Wizara kupitia Wakala wa Ufundi wa Umeme *(TEMESA)* ilamua kwa dharura kuazima injini moja toka kivuko cha Ruhuhu na kwenda kuifunga kwenye kivuko cha Kilombero ili kurejesha mawasiliano kati ya Ulanga na Kilombero. Kwa sasa injini mpya kwa ajili ya kivuko cha Kilombero tayari imenunuliwa na kufungwa kwenye kivuko cha Kilombero II. Ile ya kivuko cha Ruhuhu, tayari imesharejeshwa kwenye kivuko husika toka tarehe 9 Januari, 2012.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haikuwa na lengo la kuwadharau wala kuwabagua wananchi wanaotumia kivuko hiki ila ilikuwa njia ya dharura ya kurejesha mawasiliano yaliyokuwa yamekatika kati ya Ulanga na Kilombero wakati ambapo kivuko cha mto Ruhuhu kilikuwa hakifanyi kazi kutokana na kupungua kwa kina cha maji.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haitoi huduma zake kwa kuzingatia tabaka kwa wananchi. Kama ambavyo nimeeleza, kuondoa injini ya kivuko cha Ruhuhu kwa muda ilikuwa ni kwa ajili ya dharura ya kurejesha mawasiliano kati ya Ulanga na Kilombero.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namheshimu sana Mheshimiwa Magufuli. Lakini pamoja na hilo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka wakati tunaleta kivuko hiki pale, wananchi waliitwa, ngoma zilikuwepo na Mgeni Rasmi Rais wa Jamhuri akawepo. Lakini wakati kinang'olewa pale, Serikali imekwenda kung'oa kinyemela bila kuita wananchi wala kumwarifu Mbunge. Je, hiyo sio dharau kwa wananchi wale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wakati injini inang'olewa kwenda huko ilikokwenda, ilikuwa inafanya kazi vizuri kwa sababu ni injini mpya. Wakati inarejeshwa, injini ile haifanyi kazi na mpaka leo kivuko hakifanyi kazi. Je, hii siyo uchakachuaji ndani ya Serikali yetu?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumthibitishia sana Mheshimiwa Komba pamoja na wananchi wa eneo husika katika Wilaya ya Mbinga Mkoani Ruvuma na Ludewa Mkoani Iringa. Hakuna uchakachuaji wowote katika suala la kivuko cha Ruhuhu. Kivuko cha Ruhuhu kilipopelekwa pale kina uwezo wa kubeba tani 50. Siku za mwanzo palikuwa na kivuko pale ambacho kilikuwa na uwezo wa kubeba tani saba. Lakini ni ukweli pia usiofichika kwamba wakati wa masika (Februari hadi Mei) yaani miezi minne, kivuko cha mto Ruhuhu husimama kuanzia mwezi Februari hadi Mei, kutokana na kina cha maji na maji kusambaa kufika mpaka mita 500. Wakati wa Kiangazi ambapo huwa ni kuanzia mwezi Agosti hadi Januari, napo ni miezi minne. Kivuko cha Ruhuhu pia huwa kinasimama kwa sababu maji huwa yanapungua, yanafika mita 70. Kwa hiyo, kivuko cha Ruhuhu huwa kinafanya kazi katika mwezi Mei hadi Agosti, na ndio maana hata sasa hivi hakifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wizara yangu imepanga kutatua tatizo hili. Katika hatua za msingi za mwanzo, tumeamua katika bajeti hii, tulipanga zaidi ya Shilingi milioni 50 kwa ajili ya kutengeneza *lump* katika upande wa Ruvuma na upande wa Ludewa ili kivuko hiki kiwe kinavuka kwa muda mrefu, kisiwe kinasimama wakati wa masika na wala kisiwe kinasimama wakati wa kiangazi wakati maji yamepungua. Lakini pia tumetenga Sh. 90,000,000/= ambazo tunataka tuangalie uwezekano wa kufanya *feasibility study* na *detail design* za kutengeneza daraja ambalo litakuwa suluhisho la muda mrefu na kuondokana na masuala ya kuhangaika kwa wananchi wa sehemu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kumthibitishia Mheshimiwa na wananchi wote wa sehemu ile kwamba, hakuna uchakachuaji na ile injini iliyopelekwa Ruhuhu inafanya kazi na itaanza kufanya kazi mara tu maji yatakapokuwa yamefikia katika kimo hicho.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, maegesho kati ya Rorya-Kinesi na Mwigobero-Musoma yamekamilika kwa asilimia mia moja: Je, ni lini tutapata kivuko kwa ajili ya watu hawa ili wasipige mbizi?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la msingi lilikuwa linahusu kivuko cha Ruhuhu kule Mbinga na Ludewa. Lakini Mheshimiwa ameamua kuchomekea swali linalohusu kivuko cha Kinesi kwenda Rorya katika Ziwa Viktoria. Lakini kwa sababu taarifa tunazo, nataka kumthibitishia kwamba, ile *lump* imeshamalizika na kile kivuko ambacho kitakuwa na tani zaidi ya 85 kinaendelea kujengwa katika Mji wa Mwanza. Tunategemea mwishoni mwa mwezi huu kitakuwa kimekamilika na kikishakamilika tutapanga namna ya kwenda kukizindua katika eneo la Kinesi kwenda Rorya katika Mji wa Musoma. Kwa hiyo, napenda kuwathibitishia wananchi kwamba, kivuko kile kinaendelea kutengenezwa na kitakuwa na uzito wa tani 85.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii, nina swali kwa Mheshimiwa Waziri, kivuko cha Mto Ruhuhu kimekuwa ni kiunganishi muhimu sana kati ya wananchi wa Wilaya ya Mbinga na Ludewa na Mheshimiwa Rais kwa kutambua tatizo hilo aligundua kwamba kile kivuko hakiwezi kufanya kazi muda mrefu na badala yake akaahidi ujenzi wa daraja ambalo hamwezi kulichakachua kama mnavyochakachua kivuko hiki. *(Makofi)*

Sasa swali kwa Mheshimiwa Waziri, ukiondoa mambo ya *feasibility study,* ukiondoa mambo ya mchakato unaendelea kwa sababu bajeti yake ilikuwemo kwenye bajeti ya mwaka huu, ni lini ujenzi wa daraja la kuunganisha wananchi wa Mbinga pamoja na wa Ludewa kwenye mto huu Ruhuhu utakamilika? Tunaomba majibu thabiti na siyo majibu ya mchakato wala majibu ya *feasibility study,* naomba majibu Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga ni kuchagua na kila kitu kinapotekelezwa kinatokana na bajeti na uwezo wa Serikali na bajeti inayopitishwa na Bunge hili. Katika jibu langu la msingi na katika jibu langu la nyongeza nimeeleza kwamba kwa sasa hivi katika hatua mbalimbali ambazo zimekuwa zikichukuliwa katika daraja la Ruhuhu palikuwa na kivuko cha tani saba, ambacho kilikuwa kinaendeshwa kwa kuvutwa na kamba, hakipo *actually* kile kilizama kabisa mle kwenye maji kutokana na *terrace* ya maji na *flow* ya mto ule ambao unabeba magogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya pili pakanunuliwa kivuko cha tani 50 ambacho nacho tumepata matatizo ya kwamba wakati wa mvua upana wa *lump* zile unaongezeka hadi mita 500 wakati wa kiangazi unapungua hadi mita 70. Tumeamua kuzitengeneza zile *lump* ili kusudi kile kivuko kiwe kinafanya kazi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika hatua za muda mrefu, zimepangwa shilingi milioni 90.9 kwa ajili ya kufanya *feasibility study* ili kujenga daraja ambalo linaweza likatumika katika njia nzuri, katika mpango wa umwagiliaji katika eneo hilo pamoja na kutumika kama kivuko. Kwa hiyo, ujenzi wa barabara au wa daraja unaanza na *feasibility study,* unaingia *detail designed*, unakuja *construction*. Katika bajeti ya mwaka huu tunafanya *feasibility study* itakapofika *design* tutaleta hapa, itakapofika *construction* napo tutawajulisha na kiasi kitakachokuwa kimepangwa. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa waendelee kutumia kivuko kile wakati hatua za ku-*solve* tatizo hili zinaendelea kushughulikiwa.

Na. 91

**Ujenzi wa Barabara ya Rombo Mkuu – Tarakea kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, imefahamika kuwa, barabara ya Rombo ambayo inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami, ni nyembamba mno kwenye baadhi ya maeneo kama vile eneo la kutoka Mkuu kwenda Tarakea, sehemu ambazo ni hatari sana kwa waenda kwa miguu ambao ni wengi na tayari kumekuwa na manung'uniko juu ya hali hiyo:-

Je, Serikali inalitambua tatizo hilo, na kama inalifahamu, inachukua hatua gani kurekebisha kasoro hizo ili kunusuru maisha ya waenda kwa miguu kwenye barabara hiyo?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Rombo Mkuu hadi Tarakea yenye urefu wa kilometa 32 umekamilika. Ujenzi huo umetekelezwa na Kampuni ya *General Line for Roads and Bridges* ya Misri, ikishirikiana na Kampuni ya *Dott Service* kutoka Uganda kwa gharama ya shilingi bilioni 15.78. Barabara hiyo imejengwa kwa upana wa meta sita kwenye njia ya magari *(carriage way)* na mabega yenye upana wa nusu meta kila upande.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara hiyo umezingatia *design* ya barabara hiyo ambayo ilizingatia kwa kina mazingira yaliyokuwepo ikiwa ni pamoja na haja ya kuwapatia wananchi barabara ndefu zaidi na iliyo imara kwa fedha zilizokuwepo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchache wa magari kwenye barabara hiyo, kumekuwa na tabia kwa waenda kwa miguu na wapanda baiskeli kupita kwenye njia ya magari *(carriage way)* na hivyo kuhatarisha usalama wao. Napenda kuwashauri waenda kwa miguu na wapanda baiskeli kutumia sehemu ya mabega ya barabara kwa ajili ya usalama wao.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa ujenzi wa barabara hii umejumuisha uwekaji wa alama za barabarani zinazoelekeza mwendo sahihi kwa Madereva wanaoendesha magari kwenye miji na vijiji ambapo mwendo hautakiwi kuzidi kilometa 50 kwa saa. Hivyo, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuwakumbusha Madereva wote wajibu wa kuzingatia sheria na alama za barabarani ili kuepusha ajali.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, katika baadhi ya maeneo kama vile Mamsera, Wengwe, Keni Mkuu, tuta la barabara liko juu sana linapokutana na zile barabara za vijijini, zile *access roads,* sasa ningependa kujua kwamba hili ni tatizo katika mkataba wa ujenzi wa ile barabara au ni uzembe wa mkandarasi na hatua ambazo Serikali itachukua ili kuweza kusahihisha tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, yako maeneo kama vile Useri na Olele barabara zinazokwenda kwenye maeneo ya wananchi tena maeneo muhimu kama vile *dispensary* na kwenye Makanisa zimefungwa kutokana na ujenzi wa barabara. Tatizo hili tulishalizungumza kwenye *Road Board* pale Mkoani. Je, sasa Waziri yuko tayari kuagiza *TANROADS* Mkoa waweze kushirikiana na Mkandarasi ili kufungua barabara hizi?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge, tutawasiliana na *TANROAD* kuangalia yale maeneo ambayo yanaleta mikwamo na hasa katika kutengeneza *fider roads* zinazoenda kwenye maeneo muhimu, tuangalie ni kwa namna gani yataweza kushughulikiwa na Wizara yangu na hasa kwa kuzingatia kwamba mkandarasi bado yuko kwenye *site*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, mkitazama saa yetu na bado tuna maswali, mniwie radhi, Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 92

**Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia – Mbeya**

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya Tamko la Mheshimiwa Rais la kuzipandisha hadhi Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kuwa Chuo Kikuu bado inakabiliwa na tatizo la fedha hali inayofanya mchakato wa zoezi hilo kuwa gumu.

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuimarisha zoezi hilo la utekelezaji wa miundombinu ili kuendana na teknolojia ya kisasa katika ukanda huu wa Afrika Mashariki?

(b) Je, ni lini Serikali itakipa Chuo hicho vifaa vya kisasa vya maabara na karakana zake ambavyo hivi sasa ni vichache na mitambo mingi imechakaa?

**NAIBU WAZIRI MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Manjelwa, Mbunge wa Viti Maalum Mbeya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatoa kipaumbele kikubwa kuziendeleza taasisi zake za Sayansi na Teknolojia Mbeya ili ziwe chachu za kukua kwa uchumi na kuondoa umaskini nchini. Aidha, katika kuboresha suala la miundombinu, Serikali imekuwa ikiwekeza hatua kwa hatua katika kuimarisha miundombinu ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya ili iweze kuendana na hadhi mpya ya kuwa Chuo Kikuu hapo itakapokuwa tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilieleze Bunge lako Tukufu, hatua iliyofikiwa katika kutekeleza maelekezo ya kuibadili Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kuwa Chuo Kikuu kama ifuatavyo:-

(i) Majadiliano ya awali kati ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania *(TCU)* na uongozi wa Chuo cha Mbeya kwa ajili kupata usajili wa Chuo Kikuu imefikia katika hatua ya juu sana.

(ii) Tume imetoa mwongozo wa mahitaji ya lazima ili Taasisi ipate usajili wa awali ambayo ni pamoja na kuwasilisha rasimu ya ithibaki ya Chuo yaani *Draft Charter,* mpango mkakati wa chuo yaani *strategic plan, Tange Scheme of Service* na Muhtasari wa Chuo ambao ni *Prospectus*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuboresha miundombinu ya Taasisi ya Teknolojia Mbeya, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabweni ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800, vifaa vya mabweni, maabara ya fizikia na kemia na kadhalika.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili yenye kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa kuwa Taasisi hii inakabiliwa na changamoto ya kuwalipa wananchi fidia ambao walikuwa wametengewa maeneo kwa ajili ya upanuzi wa Taasisi hii na wananchi hao wa Mbeya hawajalipwa hadi leo, je, Taasisi ama Serikali, Waziri atuambie hapa, ina mkakati gani katika kuwalipa fidia wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, la pili, miezi michache iliyopita mimi nilitembelea Taasisi hii, ukweli ni kwamba *access* ya barabara kufika kwenye Taasisi hii haipo kabisa, inapita kwenye vichochoro ambavyo ni makazi ya wananchi. Naomba Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ituambie ina mkakati gani katika kuhakikisha kwamba Taasisi hii inawekewa barabara za uhakika, nashukuru? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, mkakati wa kulipa fidia, Chuo kimeona umuhimu wa namna ambavyo kinaweza kulipa fidia, lakini kutokana na mchanganyika au kutokuwa na takwimu sahihi katika eneo ambalo linatakiwa lilipwe fidia. Chuo kimeona kwamba maeneo yaliyo katika eneo lile yana miundombinu ya shule, yana miundombinu ya zahanati na eneo lenyewe ni dogo sana, kwa hivyo Wizara yangu imeona ni vizuri maeneo yale yaachiwe wananchi wayaendeleze ili tutafute eneo lingine ambalo halitakuwa na usumbufu wa kuweza kuwahamisha wananchi wengi kama ilivyo sasa hivi. Kwa hivyo, eneo ambalo tulikuwa tumeliangalia kwa mwanzoni, hatutaliangalia tena kwa ajili ya kuwafidia, wananchi waendeleze maeneo hayo na tutatafuta maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ambayo Mheshimiwa ameisema ni kweli kwamba barabara inayoenda katika Chuo hiki siyo nzuri sana lakini tunaongea na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi tuhakikishe kwamba barabara inayotoka katika barabara kuu iendayo Tunduma mpaka kufika kwenye

Chuo hicho inafanyiwa matengenezo na iweze kupitika kwa urahisi zaidi. Hiyo ni katika mikakati yetu ya kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu kitakapokuwa Chuo Kikuu kiweze kufikika kirahisi zaidi.

Na. 93

**Bei ya Pamba Nchini**

**MHE. STEPHEN J. MASELE** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia msukosuko wa uchumi kwa Dunia mwaka 2008/2009, bei ya pamba iliathiriwa kiasi cha kutishia kufilisika kwa wanunuzi wakubwa, hivyo Serikali iliamua kutoa fedha, maarufu kama *Stimulus Package* ili kuongeza bei kwa wakulima; mpaka sasa kuna kampuni zinazokidhi masharti ya kupewa fedha hizo lakini hazijapewa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kwa kuchelewa kuwalipa fedha hizo ni kudidimiza uchumi wa Kanda ya Ziwa hasa Shinyanga ambako kuna wakulima wengi wa pamba?

(b) Je, ni lini Serikali itamaliza kuwalipa fedha hizo wanunuzi hao ambao wanaendelea kulipa gharama za mikopo mikubwa ya Benki?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini, sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijachelewa kuyalipa Makampuni ya Pamba hususan ya Mkoa wa Shinyanga kufuatia mdodoro wa kiuchumi duniani wa mwaka 2008/2009 kwa sababu ilitoa *Stimulus Package* kwenye zao la pamba kuwasilisha takwimu za kiasi cha pamba walichonunua, bei walizouzia na gharama za uendeshaji kupitia kwenye benki zao. Makampuni yaliyofanya hivyo na kukidhi vigezo na hatimaye kuonekana kweli walipata hasara kutokana na mdororo huo, walifidiwa hasara waliyoipata kulingana na viwango vya hasara vilivyothibitishwa. Katika mchakato huo, jumla ya shilingi bilioni 9.3 zililipwa na Benki Kuu kwa Makampuni 15 ya Pamba yaliyokidhi vigezo kupitia Benki zao; Makampuni mengine 17 hayakulipwa kwa kushindwa kukidhi vigezo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizowasilishwa na Makampuni ya Ununuzi wa Pamba na uchambuzi uliofanyika na baadaye malipo yaliyofanyika kwa makampuni yaliyokidhi vigezo vilivyowekwa, Serikali imeridhika kwamba makampuni yote yaliyostahili malipo hayo yamelipwa na hakuna kampuni inayostahili malipo hayo ambayo bado haijalipwa.

**NAIBU SPIKA:** Jamani wamesema hakuna kampuni ambayo haijalipwa, sasa maswali ya nini tena, Mheshimiwa Stephen Masele!

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nasikitika kwa namna ambavyo Benki Kuu imeipotosha Wizara ya Kilimo, kwa kuwa Makampuni ya Jambo Ginnery, *Gaki Investment*, *NGS Investment, Vitrex, BillChild Oil, Aharm Investment* ni makampuni makubwa ya ununuzi wa pamba katika Mkoa wa Shinyanga na Mwanza, makampuni yamekidhi vigezo vyote na yaliwasilisha kwa wakati lakini mpaka tunavyozungumza hayajafidiwa na kwa kuwa Serikali haina uwezo wa kununua pamba yote inayolimwa na wakulima kama ilivyoshindwa kununua mahindi yote yaliyolimwa Sumbawanga na Songea, je, Serikali iko tayari kukaa na Bodi ya Pamba pamoja na wanunuzi hawa kupitia upya taarifa hizi na kuweka uwezekano wa kuwafidia ili wasifilisiwe na mabenki?

Kwa kuwa Serikali iliweka *commitment* ya kuwalipa watumishi wote wa Chama cha Ushirika cha *SHIRECU*, je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ya kuwalipa fidia, mapunjo ya mshahara watumishi wote wa *SHIRECU? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ninayo barua kutoka Benki Kuu kwamba makampuni yote yaliyokidhi viwango yamelipwa na hapa ninayo orodha

ambayo nitamkabidhi baadaye Mheshimiwa Mbunge inayonionyesha makampuni 15 ambayo yalikidhi vigezo na yakalipwa shilingi bilioni 9.3 na makampuni mengine 17 ambayo Benki inasema ni makampuni ambayo hayakulipwa *Stimulus Package* kutokana na kwamba hayakukidhi vigezo na kwamba pia yalitengeneza faida katika *process* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningesema kama bado makampuni hayo yanafikiri yanaidai Serikali, nafasi ipo kabisa, waje tuzungumze, pia tuzungumze na Benki Kuu kurejea mchakato mzima, kama itathibitika kwamba wao wana haki, mimi siamini kwamba Serikali itawalalia, nafikiri nafasi hiyo bado ipo, waje tuzungumze ili mahesabu hayo yapitiwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba niseme kwamba Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, nadhani inaongozwa na Mheshimiwa Zitto, ilivyopita kwenye Bodi ya Pamba siku za karibuni haikuridhishwa sana na jinsi usimamizi wa *Stimulus Package* ulivyofanywa na hivyo iliagiza kwamba *CAG* akague *process* nzima na mchakato uliotumika ili kuangalia uhalali wa malipo yaliyofanyika. Kwa hiyo, tusubiri *CAG* afanye kazi yake, nadhani matokeo yataweza sasa kutupa mwanya kwamba nini kilifanyika na nani anastahili kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *SHIRECU* na wale wengine ambao hawajalipwa, ni pamoja na *NBFACO,* naomba nirejee kusema pia nimewasiliana na Hazina wamesema kulikuwa bado kuna kasoro katika madai ya Vyama vya Ushirika ambavyo bado havijalipwa. Msimamo wa Serikali tangu zamani ni kwamba Serikali ilimua kulipa madeni yote ya Vyama vya Ushirika lakini kama kuna kasoro kasoro ndogo na nimeambiwa bado kumbe kuna Vyama vingine havijatimiza masharti basi nadhani tufanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, anayewashwa ndiye anayejikuna, sasa naomba Mheshimiwa Mbunge na hivi vyama tusingoje kuja hapa Bungeni kuuliza maswali, tuwasiliane na Wizara pamoja na Hazina tuangalie kama kweli bado kuna vyama vya ushirika vinaidai Serikali basi tutafute namna ya kulipa madeni hayo maana yake Mheshimiwa Rais mwenyewe alishaagiza kwamba tulipe madeni ya nyuma. Lakini pia aliagiza kwamba baada ya malipo hayo yote kukamilika, vyama vya ushirika ambavyo vitaendelea tena kulimbikiza tena madeni basi Serikali haitayachukua madeni mapya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bunge!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja fupi kwa Mheshimiwa Waziri.

Katika siku za awali Waziri wa Fedha alishawahi kutoa tena kwa maandishi taarifa kwamba mjadala wa *stimulus package* umefungwa lakini leo Waziri anatupa taarifa nyingine ambayo inapingana na hiyo. Tuchukue kauli ipi ambayo ni kauli sahihi ya Serikali na wakati huo huo Serikali itakuwa sasa tayari basi kuweza kuhakiki makampuni ambayo yalifaidi *stimulus package* ambayo bado yanaonekana yana utata na watu hawajui hali halisi ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba yapo makampuni ambayo hayakukidhi vigezo na Benki Kuu ilisema hayo ambayo hayakukidhi hayatalipwa na kweli Benki ikasema tumefunga mjadala huu kwa sababu hayajalipwa.

Lakini pia nikasema Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma ilipokagua hesabu za Bodi ya Pamba nimekuwa na wasiwasi kwamba huenda usimamizi wa malipo ya *stimulus package* ulikuwa kwa maneno mengine haikuridhika zaidi na nimeagiza *CAG* afanye ukaguzi kuona uhalali wa malipo hayo. Sasa ndiyo maana nimesema baada ya *CAG* kufanya ukaguzi kama itathibitika kwamba kumbe kuna uhalali wa malipo sioni ni sababu gani Serikali isirejee tena kuzungumza na watu hawa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma imegundua kwamba zaidi ya shilingi bilioni 18 ambazo zilikwenda Bodi ya Pamba kwa ajili ya kuwalipa wakulima wa pamba zililipwa kwenye kampuni hewa na zililiwa.

Lakini pili, kutokana na maswali yaliyoulizwa kwa Waziri Mkuu na baadaye Waziri wa Fedha kuna jumla ya shilingi bilioni 18 ambazo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amesema kwamba hajapewa nyaraka na Wizara ya Fedha, na Spika wa Bunge aliagiza humu Bungeni kwamba nyaraka hizo

zitoke na orodha ya watu wote waliofaidika na *stimulus package* wa thamani ya shilingi trilioni 1.7 iletwe kwenye Bunge. Mpaka sasa orodha hii haijaja.

Je, ni lini Serikali itaacha kukaidi maagizo ya Bunge? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nisaidie kujibu majibu mazuri ambayo Naibu Waziri ameyatoa.

Kwanza kabisa *rescue package* ilikuwa ni *specific* kwa mwaka 2008/2009 na ilikuwa *1.7 trillion shillings* kwa maeneo ambayo yalibainishwa. Makampuni hayakutakiwa kwenda Benki Kuu au Hazina moja kwa moja, makampuni yalitakiwa kwenda kwenye benki zao, benki zao ndiyo zitakazosema kwamba makampuni hayo kama yalipata hasara ni hasara ambayo ilitokana na msukosuko wa uchumi au hasara hiyo ilitokana na ufilisi. Serikali au Hazina haina utaalamu wa kufanya kazi hiyo lakini kazi hiyo ilikuwa inafanyika na Benki Kuu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, makapuni ambayo yalidhihirika kwamba kweli kupata kwao hasara kulitokana na msukosuko wa uchumi ndiyo hayo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba yalilipwa. Makampuni ambayo hata kama kusingekuwa na msukosuko wa uchumi yalishafilisika lakini kwa sababu kuna *rescue package* wakaja kuleta madai kwamba na wao wanahusika, Benki Kuu haikuyaidhinisha yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anachosema Naibu Waziri ni kwamba kama una *cooperatives* au mtu yeyote mwingine ambaye kweli anaridhika kwamba anayo haki na kwamba alipata hasara kwa sababu ya msukosuko wa uchumi Serikali haiwezi kufunga *chapter* yake moja kwa moja. Kampuni hiyo inaweza kupitia benki yake si kwenda Benki Kuu moja kwa moja kwa sababu haweki pesa Benki Kuu bali anaweka pesa kwenye *Commercial Bank, Commercial Bank* yake ndiyo inayojua mwenendo wa biashara yake na kwa hiyo, *Commercial Bank* ikipendekeza kwa Benki Kuu na Benki Kuu ikapendekeza kwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha bado anaweza akaruhusu pesa zikalipwa. *(Makofi)*

Sasa kuhusu maswali *specific* ambayo Mheshimiwa Zitto ameyauliza, tunayafahamu na yameletwa na tunawasiliana na *Controller and Auditor General,* nadhani itakapokuwa tayari tutaleta taarifa hiyo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Na. 94

**Gawio la Mchele Unaotoka Japan**

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA** aliuliza:-

Katika mwendelezo wa kutoa misaada ya chakula nchini kwetu Serikali ya Japan kwa mwaka 2011 imetoa tani 17,000 za mchele ambao 10% ya tani hizo hupelekwa Zanzibar:-

(a) Je, 10% ya tani hizo imeshapelekwa Zanzibar?

(b) Je, ni nini takwimu sahihi za mchele huo unaopokelewa Japan kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na nini gawio la Zanzibar kwa kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) imepokea jumla ya tani 29,725 za msaada wa mchele kutoka Serikali ya Japan na tani 2,971 kati ya hizo zilitengwa kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Utaratibu

uliokubalika ni kwamba mchele unapoingizwa nchini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapata mgao wa 90% na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapata 10%.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka mitano iliyopita, mgao ulikuwa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Mwaka 2005/2006 | - | (Hakuna msaada); |
| Mwaka 2006/2007 | - | (Hakuna msaada); |
| Mwaka 2007/2008 | - | (Tani 1,2416 na SMZ iligawiwa tani 1,241); na |
| Mwaka 2009/2010 | - | (Tani 1,7309 na SMZ iligawiwa tani 1,730). |

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida uuzaji wa mchele unafanywa kwa zabuni ambapo SMT inaitaarifu SMZ kuhusu gawio lao na SMZ ndiyo wanaopendekeza wazabuni watakaonunua mchele na kuupeleka Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 17 Februari, 2011, SMT ilipokea tani 17,039 kutoka Japan, kati ya kiasi hicho tani 1,730, sawa na 10% zilitengwa kwa ajili ya SMT na wazabuni wawili walioteuliwa walikwishachukua mchele huo. *(Makofi)*

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na jawabu zuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa huu mchele kwa upande wa Zanzibar utakuwa haupati jawabu sahihi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri lakini sisi tutakaporudi Zanzibar tutafuatilia namna gani huo mchele unapokelewa na unavyouzwa? Lakini nina maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

Je, ni vigezo gani vilivyotumika katika ugawaji wa mchele huu hadi kupelekea Zanzibar kupata 10% ya mchele wote unapokelewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mchele huu unapopokelewa huku Tanzania Bara baada ya kuuzwa *definitely* utakuwa fedha zake zinaelekezwa katika miradi ya maendeleo. Ni miradi gani ya maendeleo upande wa Tanzania Bara ambayo imefadhiliwa na fedha hizi na baada ya kufanyika miradi hiyo huwa inakaguliwa wakati gani na inakaguliwa na nani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanya, maswali mangapi hayo? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nadhani kuhusu vigezo ningemuomba Mheshimiwa Sanya tupate muda kwa sababu yapo makubaliano maalum ya jinsi ya kugawanya hiyo 10% na kwa muda ulionipa itatuchukua muda mrefu kuyapitia na kama alivyosema mwenyewe atafuatilia pia kule Zanzibar kuona mchele uliopelekwa uligawaje. Hilo siyo jukumu langu bali ni jukumu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu fedha hizi ni miradi kiasi gani ambayo imefaidika, miradi ni mingi labda kwa kifupi tu niseme kwamba mchele unapouzwa makubaliano yetu na Serikali ni kwamba fedha hizo zinawekwa katika mfuko maalum ambao tunaita *Tanzania Japan Food Aid Counterpart Fund* na miradi ambayo imeshafaidika ni mingi nikisema niorodheshe haitawezekana kwani ni fedha nyingi sana. Naomba tu kama anahitaji tupate hiyo orodha, basi hiyo tunaweza tukaitafuta kutoka kwenye utawala wa mfuko ambao upo kwenye Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi ni kwamba ukaguzi wa fedha zote za umma unafanywa kwa mujibu wa taratibu za ukaguzi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na ninakushukuru sana. Najua umuhimu wa mchele Zanzibar. Swali la mwisho linaulizwa na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole.

Na. 95

**Kuongezeka kwa Ajali Barabarani**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED** aliuliza:-

Tafiti zinaonyesha kuwa mwaka 1994 Taifa lilipoteza shilingi 11,000,000,000,/= kutokana na ajali za barabarani.

(a) Je, katika miaka mitano iliyopita Serikali imetumia kiasi gani cha fedha kutokana na kuongezeka kwa ajali hizo?

(b) Je, Serikali inawasaidiaje waathirika wa ajali hizo?

**WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007 Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini yaani SUMATRA ilianza kufanya utafiti uliohusisha tafiti zilizotangulia ukiwemo ule wa mwaka 1994 alioutaja Mheshimiwa Mbunge. Nakubali kuwa gharama za ajali mwaka 1994 zilikuwa ni shilingi bilioni 38.138 badala ya shilingi bilioni 11. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti ulioendelea kufanywa na Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini ili kubaini vyanzo vya ajali na pia hasara zinazotokana na ajali za barabarani ukizingatia gharama za uharibifu wa mali yaani magari na miundombinu, gharama za matibabu, gharama za usimamizi hali kadhalika upotevu wa nguvu kazi na utoaji wa elimu umeonyesha kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ajali zimeligharimu taifa kama ifuatavyo:-

Mwaka 2006 shilingi bilioni 508.02, mwaka 2007 shilingi bilioni 167.59, mwaka 2008 shilingi bilioni 225.71 na mwaka 2010 shilingi bilioni 849.91. Jumla ya gharama hizo ni shilingi trilioni 1.95.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata picha ya gharama kwa mfano, gharama za mwaka 2006 zilikuwa ni 3.4% ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua matatizo yanayowapata waathirika wa ajali, Serikali imeendelea na mikakati mbalimbali ya kuwasaidia waathirika wa ajali kwa kutoa elimu kwa waathirika kuhusu stahiki zao, taratibu zinazofuatwa katika kulipwa fidia na bima na namna ya uthibitishaji wa waathirika na kuimarisha vitengo vya kuhudumia wahanga wa ajali. *(Makofi)*

Aidha, ili kuhakikisha kuwa ajali zinapotokea waathirika wanafidiwa ipasavyo Serikali kupitia *SUMATRA* inahakikisha kuwa vyombo vya usafiri vinakuwa na bima inayomlinda abiria, inatoa elimu inayowawezesha abiria kuhakikisha wanakata tiketi zenye taarifa zote muhimu kama jina la msafiri, chombo cha kusafiria, tarehe na namba ya tiketi na kuhakikisha wamiliki wa vyombo vya usafiri wanazingatia haya pamoja na masharti ya leseni za usafirishaji. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani ya mwaka 2007 ilizungumza kama ifuatavyo; *"Nobody killed or serious injured due to the road traffic accident."*

Leo hii ni mwaka 2012 takribani miaka sita imepita tangu *vision* hii iweze kuzungumzwa na Serikali tunashuhudia Watanzania wenzetu wakiwa yatima, walemavu na wakipoteza mali zao. Lakini vilevile kwa majibu ya Waziri ni kwamba Pato la Taifa nalo limeendelea kuathirika kutokana na ajali za barabarani.

Je, Mheshimiwa Waziri unawaambia nini Watanzania ambao wanaendelea kuteseka na ajali hizi za barabarani na ninyi mmejiwekea *vision* ya namna hii?

Hivi karibuni katika Mkoa wa Tanga wakati wa ziara ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kulitokea ajali ambayo ilisababisha askari wetu wawili kupoteza maisha na wanne kuwa majeruhi na kupelekewa katika hospitali ya Mkoa wa Tanga. Wahanga hawa hadi sasa wapo katika hospitali ya mkoa. Mheshimiwa Waziri, kupitia kwako tunataka kuelewa ni namna gani Serikali imeweza kuwasaidia askari hawa hasa ukizingatia kwamba sasa hivi kuna mgomo wa madaktari nchi nzima? Hawa askari wanaendelea kuteseka katika hospitali hiyo. Ni utaratibu gani ambao utauchukua wa kuwasaidia wahanga hawa?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni sawa kabisa Taifa linapoweka *vision* ya kutokuwa na vifo na pia waathirika wengine katika ajali. Lakini ajali popote duniani zitazidi kuendelea tu. *Vision* kama hizi ni kukupa mfumo na mikakati ya kuona unafanya vigezo gani ili ajali zipungue. Lakini kusema utaondoa ajali moja kwa moja hiki ni kitu ambacho hakiwezekani.

Sasa katika mikakati ya kuhakikisha kuwa ajali zinapungua niwasifu hapa *SUMATRA*, hivi karibuni wamechukua mbinu kali sana na hatua kali sana kuhakikisha kuwa mwanzo walianzia na ajali, ajali ikitokea basi lile ambalo limesababisha ajali linafungiwa leseni na kwa kipindi cha Julai mpaka Desemba mwaka 2011 mabasi 101 yamefungiwa leseni kwa sababu hiyo na hayo ni mabasi ambayo yanamilikiwa na kampuni takribani 19. *(Makofi)*

Sasa hivi mikakati siyo kuishilia tu ngoja ajali itokee tu, pale tunapoona mwelekeo au *trend* kama wanavyosema wazungu, mwelekeo wa kampuni unakwenda kwenda kiajali ajali kwa maana ya kuwa wana-*practice accidents* hatutangoja mpaka *accident* itokee. Ikithibitika uzembe ambao umejitokea katika yale yaliyofungiwa yaani uzembe wa madereva na ubovu wa magari, ikithibitika hizo ndiyo sababu tutazidi kunyang'anya leseni za mabasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ni majonzi ajali zinapotokea na ajali iliyotokea Tanga ikihusisha msafara wa kiongozi ni majonzi hivyo hivyo. Kwanza, tunawapa pole wote ambao waliathirika, ilikuwa ni matumaini yangu kuwa wagonjwa wale wameshaondoka hospitali na wanatibiwa mahali ambapo panastahili. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge nitalifuatilia. Tanga nakujua, Bombo nitakujua, nitalifuatilia ili kujua ni nini ambacho kimejiri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo ya nyongeza, kwa suala la Mheshimiwa Mbunge. Kwa kawaida Askari wa Jeshi la Polisi anapopata ajali au anapopata maafa yoyote kama amefariki tuna utaratibu wa kutoa fidia kwa familia yake hasa kama muda wake wa kustaafu bado haujafika.

Lakini la pili, kwa wale ambao wanapata ajali tuna utaratibu wa kuendelea kuwahudumia na kuwapatia matibabu. Hili ndilo ambalo tunalifanya na hili ndilo jukumu la Jeshi la Polisi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa nawaomba mkae kidogo, nitawapa nafasi nimalize tu matangazo, halafu tutaendelea na miongozo.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Ukumbini mwa Spika ni pamoja na Wabunge kutoka Bunge la Afrika Mashariki ambao ni wawili nao ni Mheshimiwa Said Gharib Bilal na Mheshimiwa Sebtuu Mohammed Nassor. Waheshimiwa Wabunge karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni watatu wa Mheshimiwa Said Mussa Zubeir wakiongozwa na ndugu Salama Issa Ahmed. Karibuni sana popote pale mlipo, nawashukuruni sana. Huyu Salama ni mke wa Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, lakini pia wako watoto wake wawili Eknut Said Mussa na Mussa Said Mussa. Ahsanteni sana na karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Wako wageni wanne wa Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd wakiongozwa na Ndugu Hadharat Hilali Ame. Pia kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Hussein Amar wakiongozwa na Ndugu Sadik Falaji ambaye ni Mwenyekiti Shirika Lisilo la Kiserikali (*NGO*) OKOA SAYARI liliko Jimbo la Nyanghw'ale. Karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Biashara *(CBE)* Dodoma. Ahsante sana wanafunzi wa *CBE* Dodoma, ninyi ni majirani zetu, karibuni sana kila mnapopata fursa. *(Makofi)*

Pia wako Maafisa kutoka SUMA JKT, Maafisa kutoka Hazina na Maafisa wa Magereza, karibuni kutoka popote pale mlipo. *(Makofi)*

Vile vile tuna wanafunzi 20 kutoka Tanzania *Pharmaceutical Students' Association* (*TAPSA*). Karibuni sana Wafamasia. Pia tuna wanafunzi 48 na walimu watatu kutoka *Dar es Salaam Independent School*. Ahsante sana kwa kuja kwenu kutoka Dar es Salaam, tunapenda sana kuwaona wanafunzi hasa ninyi watoto wetu mkitembelea Bunge na kutumia fursa hii. Nialike shule nyingine pia ambazo zinapata fursa kama hii kuweza kufanya hivyo, tunawatakia safari njema tunaporudi. (*Makofi)*

Wapo viongozi Wanaharakati wa Mabadiliko Tabianchi ambao ni ndugu Ruth Christian na Ndugu Flora Julius. Karibuni sana. Katika wageni wetu kutoka Bunge la Afrika nilimsahau mmoja ambaye ni Mheshimiwa Mama Mmari. Ahsante sana na karibu sana Mheshimiwa hapa Dodoma ni kwako, karibu sana. *(Makofi)*

Mwisho sio kwa umuhimu, naomba kumtambulisha mgeni wa Mheshimiwa Catherine Magige ambaye ni ndugu James Ole Milia. Karibu sana Mheshimiwa James Ole Milia. Huyu ni Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya Umoja wa Vijana Taifa na pia ni Mwenyekiti wa Vijana wa Mkoa wa Arusha na nikisema Mwenyekiti wa Vijana wa Mkoa wa Arusha maana yake ni kwamba vilevile ndiye anayeshughulikia Arumeru Mashariki kwa Chama cha Mapinduzi. Lazima tuwatanie kidogo jamaa zetu. (*Makofi)*

Sasa nitoe matangazo ya kazi. Mheshimiwa George Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo kukutana baadaye saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa "C".

Mwenyekiti wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kukutana saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa "B". Wale wa Sheria Ndogo ni Msekwa "C" na hawa wa Ulinzi, Mambo ya Nje na Usalama ni Msekwa "B".

Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda na Biashara, anaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane vilevile saa saba chumba Na. 219, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala.

Mheshimiwa David Sillinde, Kaimu Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anaomba Wabunge wa Chama hicho wakutane baada ya Semina kutakuwa na kikao katika Ofisi ya Kambi ya Upinzani Bungeni. Hivi vikao mbona vingi sana. CHADEMA baada ya Semina kuna kikao ofisini kwao.

Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anawaomba Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji saa saba mchana kukutana katika Ukumbi Na. 227.

Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwamba wakati huo wa saa saba, mkutane katika chumba Na. 231, Jengo la Utawala, ghorofa ya pili.

Katika kutambulisha wageni kwenye jukwaa la Mheshimiwa Spika nimetonywa kwamba yupo Mheshimiwa Mzee wetu Dokta Juma Ngasongwa. Ahsante sana. Mheshimiwa Ngasongwa amekuwa Mbunge hapa kwa miaka mingi tu. Yeye amepata kuwa Waziri na sasa ni mmoja wa Washauri wetu, tunakukaribisha sana na karibu sana hapa Bungeni. Karibu sana Mheshimiwa. (*Makofi)*

Sasa kuna Semina ya Wabunge wote kuhusu Hali ya Uchumi. Katibu wa Bunge anawatangazia Wabunge wote kuhudhuria Semina Kuhusu Hali ya Uchumi ambayo itafanyika leo baada tu ya kuwa nimeahirisha shughuli hizi za Bunge katika Ukumbi wa Msekwa. Semina hiyo itaanza saa sita kamili kwa sababu watoa mada wetu wako njiani wanakuja. Sasa kwa maana hiyo, naziomba zile Kamati zote

zilizosema zitafanya vikao vyake tuhudhurie Semina ile tufanye vikao mara baada ya Semina hiyo kwisha ili sote tuweze kushiriki katika kufahamu jambo hilo la uchumi vizuri zaidi. Huu ndio ushauri ambao natoa. Baada ya hapo kuna watu walisema miongozo au ngoja nikae niwaorodheshe kwanza, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Stephen Maselle, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Charles Mwijage, kuna mwingine? Ni wanne? Tuanze na Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 47, kuliomba Bunge kujadili jambo la dharura baada ya maswali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inalo jambo la dharura sana. Hii ni karibu wiki ya pili Watanzania wenzetu wanakufa mahospitalini. Limekuwa linaombwa hapa, naomba tena leo niombe Bunge lako lijadili suala la mgomo wa Madaktari pamoja na yote yanayoendelea. Wako watu wanaosema ni kuingilia mihimili mingine hapana, wanaokufa ni Watanzania ambao leo tuko hapa kuwawakilisha. Litakuwa Bunge la ajabu sana na tutaingia kwenye historia, Watanzania wanakufa, tunasema hatuwezi kuingilia mhimili mwingine. Naomba leo Wabunge mniunge mkono ili Spika uamue sasa tuanze kujadili suala hili gumu na ambalo Watanzania wanapoteza maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba Mwongozo wako wakati nilipouliza swali Na. 85, ulinipatia fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Nilipouliza swali la nyongeza sikupatiwa jawabu. Nilichouliza na kutaka Serikali ni kuunda Tume ya kuthibitisha madhara na uonevu wanaofanyiwa watu wangu. Nilichopewa ni jibu kwamba kwa nini sijakwenda kutoa ripoti Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa naomba Mwongozo wako.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 46(1).

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Zitto ameuliza swali hapa ameuliza kama ni sahihi kwa maagizo ya Mheshimiwa Spika, kwamba taarifa waliyolipwa fedha za *Stimulus Package* iletwe Bungeni na Waziri hajajibu hilo swali. Maagizo aliyoyatoa Spika yamepuuzwa mpaka leo kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Spika, maagizo yako wewe mwenyewe kwa Mheshimiwa Majaliwa kujibu swali langu ambalo hakulijibu kikamilifu hayakutekelezwa mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo kama ni sahihi, kama inaruhusiwa na Kanuni za Bunge hili Tukufu kwa Mawaziri kupuuza maagizo yanayotolewa na Kiti chako Mheshimiwa Naibu Spika. Nashukuru sana.

**MHE. STEPHEN J. MASELLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami najielekeza kwenye Kanuni ya 68(7). Wakati nimeuliza swali langu la nyongeza kuhusiana na *Stimulus Package* kwenye jibu imeonyesha kwamba jumla ya shilingi bilioni 9.3 zimelipwa na kwa kuwa zao la pamba kwa Kanda ya Ziwa ndio uti wa mgongo wa uchumi wa nchi wa kanda hiyo, tofauti na madini ambayo tunagawana wote nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, Mheshimiwa Zitto alipouliza swali la nyongeza alisema kwamba Bodi ya Pamba imepokea jumla ya shilingi bilioni 18 na kwenye jibu hapa linaelekeza ni jumla ya shilingi bilioni 9.3. Nataka mwongozo wako kwamba tofauti ya shilingi bilioni 8.7 imelipwa kwa akina nani. Kwa kuzingatia kwamba kutowalipa fidia Makampuni hayo niliyoyataja ni kuyaweka katika hali ya kufilisiwa na Mabenki ambayo yanaendelea kulipa mikopo ambayo ni *specific* kwa kipindi kile cha mdororo wa uchumi. Pia kwa kufilisika Makampuni hayo inapelekea wananchi pia kufilisika kwa kuwa hakuna mnunuzi mwingine wa pamba zaidi ya Makampuni hayo. Naomba mwongozo wako. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge mliosimama kwa ajili ya kutaka mwongozo. Wabunge watatu mmetaka Mwongozo na Mbunge mmoja ametoa hoja.

Nikianza na la Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Maselle na la Mheshimiwa Tundu Lissu ambao karibu wote wametumia ile Kanuni ya 68(7). Mwongozo wangu ni kwamba mtupe nafasi kesho atakuwepo hapa Mheshimiwa Spika atatolea Mwongozo mahsusi kuhusiana na yote matatu ambayo mmeyatoa ili tupate muda kuyatafakari kwa leo. Lakini nisisitize tu hapa kwamba, kwa kweli agizo la Spika kuhusu kupata orodha ya wale waliofaidika na *Stimulus Package* ni agizo la kikao kilichopita cha Bunge, ni agizo ambalo linapaswa kutekelezwa mara moja. Naamini kabisa Serikali wanatusikia, lakini kama nilivyosema Mheshimiwa Spika atayazungumzia yote matatu kesho wakati wa kipindi cha maswali kitakapomalizika.

Baada ya masuala ya miongozo kwisha, sasa Mheshimiwa Serukamba ametoa hoja kuhusu suala la dharura kwa kutumia Kanuni ya 47(1) ambayo inasema: "Baada ya muda wa maswali kwisha kama ulivyokwisha sasa, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa Shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma". Hoja yake kwa kweli imeungwa mkono na jambo hili ni jambo kubwa kwa vyovyote vile sidhani kama tunaweza tukawa katika Bunge hili ukiondoa vita na jambo linalokidhi vigezo vya dharura linalozidi hili. Kwa hiyo, ni jambo ambalo kwa kweli kimsingi ni la dharura kwa vigezo vyote. (*Makofi)*

Sisi Wabunge kwa mujibu wa Ibara 63(2) ya Katiba yetu ambayo tunayo mpaka sasa ya mwaka 1977 inasema wazi kwamba: "Bunge hili litakuwa ndio chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyombo vyake vyote…". Sasa huwezi kusimamia jambo au huwezi kuwa mshauri mzuri kama hujapata ukweli au hujapata kidogo undani wa mambo na ndio maana jambo hili mliposimama mara ya kwanza, tena mkasimama, tukashauri kwamba ni vizuri liende katika Kamati yetu ili tutakapoishauri Serikali, tukiwashauri hawa Watumishi wa Serikali, tuwe tunatoa ushauri ambao unatokana na watu ambao wako *informed.*

Japo kuna baadhi ya watu wanatafsiri kwamba jambo hilo ni kuingilia Serikali, si kweli hata kidogo. Tutakuwa ni Bunge la ajabu sana ambalo hali kama hii inatokea, tumekaa tu hatueleweki, nchi nzima itatushangaa na sasa tumebakiza siku mbili tuondoke hapa. Tukiondoka hapa kimya katika hali ilivyo kila mtu atatushangaa. Kwa hiyo, baadhi ya magazeti yamepotosha kidogo alichokisema Mheshimiwa Spika, Anne Makinda jana. Yameandika kwamba Mheshimiwa Spika, amepiga marufuku kujadili *issue* hii Bungeni. Mheshimiwa Spika hakufanya hivyo, yeye alisema tuwe na subira, Kamati yetu tuliyoipa ile kazi iweze kurudi, ituletee upande wa pili wa nini ambacho kinaendelea. Kwa sababu sasa amesimama Mbunge kwa mara ya sita. Alisimama Mbunge siku ya kwanza kwa suala hili, akasimama Mbunge siku ya pili kwa suala hili hili, akasimama Mbunge kwa mara ya tatu kwa suala hili hili. Ijumaa iliyopita mara ya nne kwa suala hili hili na jana mara ya tano kwa suala hili hili na leo mara ya sita kwa suala hili hili. Ni vigumu sana Meza sasa kuendelea kunyamaza kuhusiana na jambo hili, ni vigumu sana. (*Makofi)*

Lakini kwa uendeshaji bora Shughuli za Bunge, Mheshimiwa Spika anashauriwa na Kamati yake ya Uongozi. Kwa hiyo basi, naiomba Kamati ya Uongozi wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati zetu za Bunge tulioko hapa mara tu tukitoka, tukutane pale kwenye Ukumbi wa Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Spika, yupo ili tuweze kulitazama jambo hili na tuweze kushauriana na Serikali kwa haraka. Kwa maana hiyo, kwa wakati muafaka tutawasiliana kuhusu namna ya kuenenda kuhusiana na jambo hili. (*Makofi)*

Katika kumalizia, wito wangu, wito wa Mheshimiwa Spika na wito wa Wabunge wote, ni kuwataka ndugu zetu Madaktari popote pale walipo, nchi nzima warudi kazini na kuitaka Serikali kuendeleza juhudi zake za kujaribu kuangalia kwamba jambo hili linamalizika kwa salama na amani. Nina hakika Serikali inalifanyia kazi kwa undani na kulipa umuhimu wa hali ya juu sana. Tujitahidi ili kuokoa maisha ya watu wetu.

Hapa ndio mwisho wa shughuli za asubuhi ya leo. Baada ya matangazo haya, niwakumbushe Wabunge kuhusu Semina ambayo itaendelea muda mfupi baada ya hapa na kwa jinsi hiyo basi, naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 5.25 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 9 Februari, 2012 saa tatu asubuhi)*